# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# HOTUBA YA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI

MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM)

# KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**MEI, 2022**



**MHE. DKT. HUSSEIN ALI MWINYI**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**



**MHE.MUDRIK RAMADHAN SORAGA**
**WAZIRI WA NCHI AFISI YA RAIS -KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**



**BI KHADIJA KHAMIS RAJAB**
**KATIBU MKUU**
**KAZI NA UWEZESHAJI**
**AFISI YA RAIS- KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**



**DKT.HABIBA HASSAN OMAR**
**KATIBU MKUU**
**UCHUMI NA UWEKEZAJI**
**AFISI YA RAIS- KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**

# YALIYOMO

YALIYOMO.............................................................................................. i
VIFUPISHO VYA MANENO...............................................................................iv
1.0 UTANGULIZI.....................................................................................1
2.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI).... 6
2.1 MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022...........6
2.1.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)........................................... 6
2.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)................................................................................. 7
2.3 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)..................................................................................8
3.0 MAFUNGU YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI............10
4.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)..................................................................................12
4.1 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE...............................12
4.1.1 Programu ndogo SA070201: Uratibu wa upatikanaji wa Ajira za Staha ....................................................................12
4.1.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini..........................................................................................15
4.1.3 Programu Ndogo SA070203: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini ..............................17
4.2 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI 22
4.2.1 Programu ndogo SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.....................................................................................22
4.2.2 Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika...............................................................28
4.2.3 Programu Ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi............................34

4.3 PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI....................................................41
4.3.1 Programu ndogo SA070501: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi....................................................................41
4.3.2 Programu Ndogo SA070502: Utawala Uendeshaji........................48
4.3.3 Programu Ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.............................................................51
5.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)..........................................................................57
5.1 PROGRAMU KUU: PA0801 KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI.........57
5.1.1 Programu ndogo SA080101: Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi............................................................57
5.1.2 Programu ndogo SA080102: Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji...................................................................59
5.2 PROGRAMU KUU PA0802: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI KATIKA UCHUMI NA UWEKEZAJI...................................................64
5.2.1 Programu ndogo SA080201: Utawala na Uendeshaji....................64
5.2.2 Programu Ndogo SA080201: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi....................................................................66
5.2.3 Programu Ndogo SA080203: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba..........................................................71
6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI).................72
6.1 FUNGU A07 KAZI NA UWEZESHAJI..................................................72
6.2 FUNGU A08 UCHUMI NA UWEKEZAJI...............................................74
7.0 HITIMISHO..........................................................................................75
8.0 VIAMBATANISHO...............................................................................78

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| ARKUU | Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CUZA | Cooperative Union of Zanzibar |
| IMF | International Monetary Fund |
| NEET | Not in Education Employment and Training |
| NGOs | Non-Govermental Organization |
| PBZ | People Bank of Zanzibar |
| PPP | Public Private Partnership |
| SACCOS | Saving and Credit Cooperative Society |
| SDGs | Sustanable Development Goals |
| SUZA-IoT | SUZA - Institute of Tourism |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TIC | Tanzania Investment Centre |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TUICO-Z | Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers |
| UAE | United Arab Emirates |
| USAID | United State Agency for International Development |

| | |
|---|---|
| ZANEMA | Zanzibar Employers Association |
| ZAPSWU | Zanzibar Public Service Workers Union |
| ZASCCU | Zanzibar Saving and Credit Cooperative Union |
| ZATU | Zanzibar Teacher Union |
| ZATUC | Zanzibar Trade Union Congress |
| ZBC | Zanzibar Broadcastin Cooperation |
| ZBPRA | Zanzibar Business and Property Registration Agency |
| ZEEF | Zanzibar Economic Empowerment Fund |
| ZFDA | Zanzibar Food and Drugs Agency |
| ZIPA | Zanzibar Investment Authority |
| ZNBC | Zanzibar National Business Council |
| ZRB | Zanzibar Revenue Board |
| ZTBI | Zanzibar Technology and Business Incubator |
| ZUPHE | Zanzibar Union of Public and Health Employees |

## 1.0 **UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako likae kama Kamati ya Matumizi ili iweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa napenda kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) kwa kutujaalia uhai na uzima na kuweza kukutana hapa leo kujadili Bajeti ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Baada ya Kumshukuru Allah, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuiongoza Nchi yetu kwa amani na utulivu. Katika kipindi hichi wananchi wa Zanzibar wameweza kushuhudia maendeleo makubwa hasa katika kuimarisha miundo mbinu mbali mbali ambayo ni hatua ya kufikia maendeleo endelevu. Aidha, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kasi yake ya kuendeleza Uchumi wa Buluu Nchini, jambo ambalo litapelekea vijana kuwa na ajira za kutosha na kuweza kujitegemea. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa mapenzi kwa Wananchi wake na kutenga fedha karibu Bilioni 81 kuwawezesha Wananchi Kiuchumi; fedha ambazo zimeleta matumaini makubwa ya kuwakwamua Wananchi Kiuchumi. Hii inaonesha ni namna gani anavyoguswa na maendeleo ya nchi na wananchi wake.

3. **Mheshimiwa Spika**, Nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman na Mheshmiwa Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kufanya kazi bega kwa bega na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia na kumshauri katika masuala mbali mbali ya kuiletea maendeleo Nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kukupongeza Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kuliongoza Baraza kwa umahiri na ufanisi mkubwa kwa mwaka wa pili sasa katika awamu hii ya nane. Pia, napenda kumpongeza Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kulitumikia Baraza kwa weledi na kukusaidia Mheshimiwa Spika katika kazi ya kuliongoza Baraza hili. Aidha, Nawapongeza Wajumbe wote kwa kuendelea kushika nafasi hizi muhimu kwa maendeleo ya jamii yetu. Natumai wananchi wameanza kufaidika na kazi zenu ambazo mnazifanya katika kuwawakilisha katika chombo hichi muhimu na huduma mbali mbali mnazozitoa za maendeleo katika majimbo yenu.

5. **Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Wafanyakazi wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Mwenyekiti hodari, Mwanamama Shupavu Mheshimiwa Sabiha

Filfil Thani na Wajumbe wake wote pamoja na Makatibu wao kwa kuwa karibu sana na Afisi kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu. Pia, napenda kuwapongeza Wajumbe Wapya walioingia kutokana na teuzi zilizofanywa na vilevile, tunawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Uchumi waliopata uteuzi wa kuwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Hamza Hassan Juma aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Mheshimiwa Juma Makungu Juma aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Mheshimiwa Nadir Abdullatif Yusuf Alwardy aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Tunamuomba Allah awajaalie kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, uadilifu, busara na haki.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee Kamati hii imeendelea kuishauri Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji na kuipa miongozo ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni imani yetu kuwa Kamati itaendelea kutupa mashirikiano ya kufanikisha utekelezaji wa malengo na majukumu ya Afisi pamoja na kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Dira 2050, Sera na Ahadi za kitaifa, kikanda na kimataifa zenye nia ya kuwainua wananchi kiuchumi, kuzalisha ajira hasa kwa vijana, kuimarisha uwekezaji nchini ili kuleta maendeleo endelevu katika Nchi yetu.

7. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imeanzishwa kwa lengo la kusimamia masuala ya uwekezaji nchini; kusimamia utekelezaji wa Sheria na miongozo ya kazi; kuratibu upatikanaji wa ajira za staha hasa kwa vijana; kuimarisha program za kuwawezesha wananchi kiuchumi; kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na kuimarisha mashirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. Afisi ina jumla ya Idara 8 (Kamisheni ya Kazi; Ajira; Usalama na Afya Kazini; Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Wananchi Kiuchumi; Maendeleo ya Vyama vya Ushirika; Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Uendeshaji na Utumishi; Mipango, Sera na Utafiti), Ofisi Kuu Pemba na taasisi zinazojitegemea 2 (Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEF)

8. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ilijiwekea malengo yafuatayo:-

    1. Kukuza na kusimamia Uwekezaji kwa Maendeleo ya Nchi;

    2. Kubuni fursa za ajira nchini na kusimamia upatikanaji wa ajira za staha hasa katika Sekta Binafsi;

    3. Kusimamia utekelezaji wa Mikataba, Sheria na Kanuni za Kazi za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na kuimarisha mahusiano mazuri ya Kazi miongoni

mwa Serikali, Sekta Binafsi, Waajiri na Vyama vya Wafanyakazi;

4. Kuimarisha Usalama na Afya kazini;
5. Kukuza na kusimamia Maendeleo ya Vyama vya Ushirika;
6. Kuimarisha na kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
7. Kukuza na kuimarisha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi;
8. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Programu na Tafiti zinazohusiana na masuala ya Kazi, Ajira, Uwekezaji, Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Uwezeshaji;
9. Kuimarisha uratibu, mashirikiano, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Afisi pamoja na kuelimisha jamii juu ya shughuli za Afisi kupitia Mfumo wa TEHAMA; na
10. Kuimarisha ufanisi wa kiutendaji na maslahi ya Wafanyakazi wa Afisi.

**9. Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo, sasa naomba uniruhusu niwasilishe utekelezaji wa Programu za Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 2.0 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## 2.1 MUHTASARI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### *2.1.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)*

**10. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ilitarajiwa kukusanya mapato ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Thalathini na Tano, Laki Sita Ishirini na Sita Elfu (Tshs. 2,835,626,000) kutokana na ada za usajili na ukaguzi wa vyama vya ushirika, ada ya ukaguzi wa mikataba ya ajira nje ya nchi, ada ya ukaguzi wa maeneo ya kazi na vibali vya kazi. Kwa Kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Afisi ilitarajiwa kukusanya Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Hamsini na Tano, Laki Moja Ishirini na Sita Elfu (Tshs.2,155,126,000). Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2022, Afisi ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Hamsini na Nne, Laki Tatu na Elfu Saba, Mia Sita Tisini na Sita (Tshs.1,054,307,696) kutokana na ada za usajili, ada ya ukaguzi wa vyama vya ushirika na vibali vya kazi ambayo ni sawa na asilimia 49 ya makadirio ya makusanyo kwa miezi 9 na asilimia 37 ya makusanyo kwa mwaka. **(Kiambatanisho nambari 1 kinahusika).**

## 2.2 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

**11. Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Mia Tano Kumi na Tatu, Laki Nne Tisini na Mbili Elfu, Mia Sita Arobaini (Tshs.15,513,492,640). Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili Thalathini na Sita na Laki Tisa (Tshs.2,236,900,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote; Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tano Thamanini na Nne, Laki Sita Sabini na Sita Elfu (Tshs. 6,584,676,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Sita Tisini na Moja, Laki Tisa Kumi na Sita Elfu, Mia Sita Arubaini (Tshs.6,691,916,640) ni kwa ajili ya kutekeleza Program ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji.

**12. Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Afisi ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Mbili Tisini na Tisa, Laki Nne Sitini na Saba Elfu na Ishirini na Tano (Tshs.7,299,467,025). Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2022, fedha zote zilizoingizwa kwa matumizi ni Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tano Sabini na Sita, Laki Tisa Tisini na Tatu, Mia Tisa Sitini na Sita (Tshs.4,576,993,966) ambayo ni sawa na asilimia 63

ya utekelezaji wa Program zote kwa kipindi hicho. Kati ya hizo Shilingi Milioni Mia Saba na Sita, Laki Moja, Mia Moja na Thalathini (Tshs.706,100,130) zilitumika kwa ajili ya kutekeleza Program ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote ambayo ni sawa na asilimia 50 ya fedha kwa Program hiyo. Shilingi Milioni Mia Saba Hamsini na Tisa, Laki Nne Thamanini na Mbili, Mia Tisa Thalathini na Sita (Tshs.759,482,936) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ni sawa na asilimia 44 na Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja Kumi na Moja, Laki Nne Elfu Kumi na Mia Tisa (Tshs.3,111,410,900) zilitumika kutekeleza Program ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji sawa na asilima 75 ya fedha za Program hiyo kwa kipindi hicho **Kiambatanisho nambari 2(a) kinahusika.**

## 2.3 MUHTASARI WA MATUMIZI KWA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

**13. Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Mbili Tisini na Nne, Laki Nne Sitini na Mbili, Mia Moja Thalathini (Tshs.10,294,462,130); Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Saba

na Saba, Laki Tatu Ishirini na Mbili Elfu, Mia Moja na Thamanini (Tshs.9,707,322,180) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Shilingi Milioni Mia Tano Thamanini na Saba, Laki Moja Hamsini Elfu (Tshs.587,150,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

**14.** **Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022, Afisi ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Sitini na Tatu, Laki Saba Sitini na Mbili Elfu na Arubaini na Moja (Tshs.9,063,762,041). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2022, fedha zilizoingizwa kwa matumizi kwa fungu A08 ni Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita Hamsini na Mbili, Laki Nane Ishirini Elfu, Mia Sita Arubaini (Tshs.1,652,820,640) ambayo ni sawa na asilimia 18 ya utekelezaji wa Programu zote kwa kipindi hicho. Kati ya hizo Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Sabini na Nane, Laki Nane Ishirini Elfu, Mia Sita Arubaini (Tshs.1,378,820,640) ziliingizwa kwa matumizi ya Programu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambayo sawa na asilimia 16 ya makadirio na Shilingi Milioni Mia Mbili Sabini na Nne Elfu (Tshs.274,000,000) zilitumika kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambazo sawa na asilimia 67 ya makadirio **Kiambatanisho nambari 2(b) kinafafanua.**

# 3.0 MAFUNGU YA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

**15. Mheshimiwa Spika;** Afisi ina mafungu mawili tofauti ya matumizi ambayo ni fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ambalo lina Programu Kuu 3 na Programu Ndogo 9 na fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) lenye Programu Kuu 2 na Programu Ndogo 4. Mafungu hayo yamegawika katika Programu zifuatazo:-

### *3.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)*

| |
|---|
| **PA0702: Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote.** |
| SA070201: Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha. |
| SA070202: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini. |
| SA070203: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimatatifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini |
| **PA0703: Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.** |
| SA070301: Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. |
| SA070302: Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika |
| SA070303: Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. |
| **PA0705: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.** |
| SA070501: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi |
| SA070502: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA070503: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba |

### *3.2 FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)*

| |
|---|
| **PA0801: Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi** |
| SA080101: Programu Ndogo ya Mashikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi |
| SA080102: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji |
| **PA0802: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.** |
| SA080201: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji |
| SA080202: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi |
| SA080203: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba |

Utekelezaji wa Programu hizi umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025; Dira ya maendeleo 2050; Mkakati wa Maendeleo wa Zanzibar pamoja na Mpango Mkakati wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

### 4.1 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE

**Matokeo ya Muda Mrefu**: Kuwepo kwa Sehemu za Kazi zinazokidhi Viwango vya Usalama na Afya.

#### 4.1.1 Programu ndogo SA070201: Uratibu wa upatikanaji wa Ajira za Staha

**16. Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo ya (SA070201) ya Uratibu na Upatikanaji wa Ajira za Staha ina lengo la Kuimarisha masuala ya Usalama na Afya kwa kipindi cha mwaka 2021/2022, Programu imetekeleza yafuatayo:-

1. Inaendelea kuratibu Mafunzo ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana ili kuweza kuajirika (kujiajiri au kuajiriwa), kwa upande wa Mafunzo kazi (Apprenticeship) Afisi inashirikiana na SUZA-IoT ambapo Vijana 36 (wanaume 23 na wanawake 13) wanaendelea na Mafunzo hayo katika Sekta ya Hoteli katika fani za 'front Office Operation', Huduma za Vinywaji, Huduma za Chakula na ' House keeping na Laundry'.
2. Kwa upande wa Mafunzo ya muda mfupi (NEET Program), Afisi imefanya usaili wa Vijana ambapo

Vijana 90 (wanaume 45 na wanawake 45) wanatarajiwa kuanza mafunzo yao mwanzoni wa mwezi wa April, 2022 katika Skuli ya Sekondari na Ufundi - JKU katika fani tatu (3) ambazo ni Ushoni, Ufundi Mafriji na Vipoza Hewa, na Useremala.

3. Imetoa mafunzo juu ya fursa za Ajira kwa vijana 400 (Wanaume 116 na Wanawake 284) wa Mabaraza ya Vijana ya Wilaya zote za Unguja wamenufaika na mafunzo hayo. Pia, mafunzo juu ya fursa za ajira na umuhimu wa kujiajiri yametolewa kwa vijana 20 (Wanaume 8 na Wanawake 12) na vipindi vya kuelimisha jamii juu ya Ajira za Staha vimetayarishwa na kurushwa hewani.

4. Imeratibu upatikanaji wa Ajira 5,700 (Wanaume 3,160 na Wanawake 2,540) katika Sekta Binafsi ndani ya nchi ambapo mikataba yote ya ajira hizo imethibitishwa na Kamisheni ya Kazi kwa mujibu wa Sheria. Ajira hizo zinajumuisha Skuli Binafsi, Hoteli na Viwanda. Aidha, imeratibu upatikanaji wa Ajira 431 (Wanaume 257 na Wanawake 174) nje ya nchi katika nchi tofauti ikiwemo Oman, Qatar, UAE, Syshelles, Maldives, Kuwait, Yemen na Saudi Arabia.

5. Imeratibu shughuli za Uwakala Binafsi wa Ajira ambapo Taasisi 2 mpya zimeweza kupatiwa leseni baada ya kutimiza vigezo na masharti yaliyopo. Taasisi hizo ni IBS Company Limited

na One Stop Zanzibar Limited. Aidha, imeweza kukagua Taasisi moja ambayo ni Hilmi Manpower Company Limited iliopo Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja ambayo inaomba Leseni ya Uwakala Binafsi wa Ajira. Taasisi hiyo imeweza kupewa maelekezo kwa ajili ya kurekebisha ili kuweza kupatiwa Leseni.

6. Imeshiriki katika kikao muhimu cha mashirikiano baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Qatar kujadili utekelezaji wa Mkataba wa Makubaliano baina ya Tanzania na Qatar ambao unasimamia Wafanyakazi wanaokwenda nchini Qatar kufanya kazi. Mkutano huo ulitoa maazimio ya kwamba Mikataba ya Kazi kutoka Qatar iongezwe lugha ya Kiswahili ili kuweza kufahamika vizuri na Mfanyakazi anapokwenda kufanyakazi. Aidha kupatikana kwa wafanyakazi wenye vigezo vinavyohitajika na waajiri kupitia Taasisi za Uwakala Binafsi wa Ajira.

**17. Mheshimiwa Spika**; Program ya Uratibu wa upatikanaji wa Ajira za Staha kwa mwaka wa fedha 2022/23, imepanga kutoa mafunzo kazi ya muda mfupi ya kukuza ujuzi kwa vijana Wasiotambuliwa na Mfumo wa Elimu, Wasio na Ajira na Hawapo katika Mafunzo (Not in Education, Employment and Training). Aidha, Program imepanga kutoa fursa kwa vijana waliohitimu katika vyuo mbali mbali ambao hawana ajira kujiunga na Taasisi tofauti kwa ajili ya kupata uzoefu wa kazi (Internship). Vile

vile, Program itaendelea kuimarisha mashirikiano na wadau wa nje na ndani katika kutafuta fursa za ajira kwa vijana na kukusanya taarifa na takwimu za Ajira nchini.

18. **Mheshimiwa Spika**; Ili Program ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naliomba Baraza lako kuidhinisha ruzuku ya jumla Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini (Tshs.150,000,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 4.1.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.

19. **Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo ya (SA070202) ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini ina lengo la Kuimarisha masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 imetekeleza yafuatayo:-

    1. Imefanya ukaguzi kwenye sehemu za kazi 209 (Unguja 149 na Pemba 60) na kutoa miongozo kwa waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa kuweka mazingira bora ya Usalama na Afya Kazini ili kujikinga na matukio ya ajali na maradhi katika maeneo ya kazi.

    2. Imetoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kwenye maeneo ya kazi katika taasisi 70 (47 Unguja na

23 Pemba) kuhusiana na masuala ya usalama na afya kazini na jinsi ya kujikinga na ajali na maradhi yatokanayo na kazi.

3. Imefanya uchunguzi wa matukio ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi katika sehemu (7) za kazi ambazo zilizoripotiwa na imeonekana kuwa sababu kubwa ya matukio hayo ya ajali ni uchache wa vifaa vya kujikinga pamoja na uelewa mdogo wa usalama na afya kazini juu ya hatari zinazowazunguka na jinsi gani ya kujikinga ili zisitokee na pindi zikitokea jinsi gani ya kukabiliana nazo.

4. Imefanya usajili wa sehemu za kazi 77 (50 Unguja na 27 Pemba) kwa lengo la kuzitambua zipo katika maeneo gani na zinafanya shughuli gani ili ziweze kufikiwa kwa urahisi kwa lengo la ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini. Vile vile, imefanya tathmini ya madhara yanayoweza kutokea ili kuweka mbinu za kukabiliana nayo.

**20.** **Mheshimiwa Spika**, Program ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini kwa mwaka wa fedha 2022/23, imepanga kuimarisha utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini; Kukuza uelewa wa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa jumla juu ya Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005; Kusimamia sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa zinafuata na kutekeleza sheria, kanuni na miongozo ya Usalama na Afya Kazini; Kuimarisha uwezo wa Idara ili kuiwezesha

kutekeleza majukumu yake ipasavyo; na Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini. Pia, itafanya ukaguzi wa sehemu za kazi 240 na kufanya usajili wa sehemu za kazi 120; Itatoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi 200 (120 Sekta ya Umma na 80 Sekta Binafsi) wawakilishi wa usalama na afya kazini na Itatoa elimu juu ya hatari zinazoweza kutokea katika sehemu za kazi na namna ya kuzikabili.

**21. Mheshimiwa Spika**; Ili program ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naliomba Baraza lako kuidhinisha ruzuku ya Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini (Tshs.150,000,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 4.1.3 Programu Ndogo SA070203: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini

**22. Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo ya (SA070203) ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini ina lengo la kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa Sheria za Kazi. Pia, Programu ina lengo la kusimamia viwango vya kazi vya kitaifa na majadiliano ya pamoja ya kazi ili kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa Sheria za Kazi katika Sekta Binafsi na Sekta ya

Umma. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu imetekeleza shughuli kuu zifuatazo:-

1. Imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi mia mbili tisiini na nne (294) (Unguja 240 na Pemba 54), ili kuangalia utekelezaji wa sheria za kazi nchini. Ukaguzi huo unafanyika ili kusimamia ipasavyo Sheria zote za Kazi kwa taasisi za sekta binafsi hapa Zanzibar.

2. Imefanya ukaguzi maalum wa kufuatilia ulipaji wa kima-kipya cha chini cha mshahara wa Shilingi Laki Tatu za kitanzania (TZS 300,000/=) kwa Taasisi mia mbili na thelathini na mbili (232). Katika ukaguzi huo maalum imebainika kuwa Taasisi Mia Mbili Kumi na Tatu (213) kwa Unguja na Pemba zinaendelea kulipa kima kipya cha chini cha mshahara kilichotangazwa na Taasisi kumi na tisa (19) bado hawajatii sheria hiyo. Kamisheni ya Kazi imewataka waajiri wote kufuata Sheria za Kazi ipasavyo na kutotafuta visingizio vyovyote vya kukwepa kulipa kima hicho cha mshahara na endapo wataendelea kutotekeleza hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

3. Imewapatia vibali vya kazi wafanyakazi wa kigeni 1,863 kutoka Mataifa mbali mbali kama vile; (Afika Kusini, Kenya, Britain, Zambia, Ujerumani, Yemen, Marekani, Sudan, Canada n.k) kuweza kufanya kazi nchini. Wafanyakazi waliopatiwa vibali hivyo ni kutoka sekta Binafsi na Sekta za Umma ambazo ni;- (Mahoteli, Skuli, Utalii,

sehemu za Ujenzi, tassisi zisizo za kiserekali (NG'O), Sehemu za Afya n.k).

4. Imethibitisha Mikataba ya kazi elfu sita mia tatu na kumi na sita (6,316) (Unguja 5,501 na Pemba 815) kwa wafanyakazi wazalendo (locals) ili kuhakikisha inaendana na sheria za kazi ikiwa ni miongoni mwa haki yao ya msingi kwa mujibu wa Sheria za Kazi. Wakati wa uthibitishwaji wa mikataba hiyo wafanyakazi husika husomewa mikataba hiyo na Maafisa Kazi ili kupata uelewa mzuri juu ya haki zao.

5. Kupitia kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi – Migogoro iliyowasilishwa ni mia moja thelathini na tatu (133), iliyomalizika katika ngazi ya Usuluhishi ni hamsini na tisa (59), Migogoro iliyomalizika katika ngazi ya Uamuzi ni saba (7), Mgogoro uliokwenda mahkamani ni mmoja (1), inayoendelea na ngazi ya usuluhishi (Mediation) ni kumi na nane (18), migogoro iliyofutwa ni mitatu (3), migogoro inayoendelea katika ngazi ya Uamuzi (Arbitration) ni arubaini na tano (45). Migogoro yote hiyo iliyowasilishwa inahusu kukatishwa mikataba ya Kazi kwa wafanyakazi, kutokulipwa kwa kiwango cha mshahara stahiki kwa mujibu wa sheria, na kufukuzwa kazi.

6. Imefanya ukaguzi katika vyama sita (6) na maeneo manane (8) ambayo ni ZAPSWU sehemu ya Suza na Maruhubi (Chuo cha Utalii), COTWU-Z head

office, ZATU head office, ZAFICOWU sehemu ya SGA security Company, na Security Master Co-operation, ZUPHE head office na Afisi kuu ya TUICO (Z). Ukaguzi huo umebaini kuwa vyama vyote hivyo vinafanya kazi zake kulingana na Katiba za Vyama vyao zinavyoelekeza ikiwemo kufanya vikao vya chama kikatiba, kuhifadhi kumbukumbu za chama na kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Mrajis wa Vyama vya Wafanyakazi.

7. Imetoa elimu ya Sheria za Kazi kwa Taasisi Kumi na Sita (16) (Unguja 6 na Pemba 10). Vile vile, imerusha vipindi Sabini na Moja (71) vinavyohusiana na elimu ya Sheria za Kazi kupitia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo; Habari FM, Kati FM, Adhana FM, Assalam FM, na Mtegani FM. Lengo hasa la utoaji wa elimu ni kuwapa uelewa kwa waajiri na wafanyakazi juu ya Sheria za Kazi na haki, wajibu pamoja na stahiki zao wanapokuwa katika maeneo yao ya kazi.

8. Imefanya ukaguzi katika maeneo ya Kusini Unguja na Wilaya ya Kati na kubaini tatizo la Ajira za watoto bado linaendelea katika sehemu sita (6) ambazo ni kama:- kusini Unguja maeneo ya Kizimkazi Mkunguni, Kizimkazi Dimbani na Paje. Wilaya ya Kati maeneo ya Chwaka, Marumbi na Uroa. Kazi wanazofanyishwa watoto hawa ni pamoja na uparaji wa samaki, kutembeza watalii, kukosha gari, kutanda vitanda vya Kamba na kujishughulisha na mambo ya uvuvi. Afisi inandaa

Programu maalum ya kuziwezesha familia na kuwatoa watoto katika ajira kwa kuwarejesha skuli au kuwawezesha kwa ambao hawawezi kurudi skuli kutokana na umri.

23. **Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2022/2023**,** Kamisheni ya Kazi kupitia Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja mbali na majukumu mengine itafanya ukaguzi kwa Taasisi Mia Saba (700) (Unguja 600 na Pemba 100), Itathibitisha mikataba ya kazi kwa wazalendo elfu tano (5,000) (Unguja 4,000 na Pemba 1,000), Itakagua vyama vya wafanyakazi na waajiri kumi na nne (14), itatoa elimu ya Sheria za Kazi kwa taasisi thalathini (30) na itarusha vipindi ishirini (20) kupitia vyombo vya habari.

24. **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023; naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Ishirini na Tisa (Tsh.1,229,000,000) kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

25. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu **(PA0702)** ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote kwa kipindi cha Julai – Machi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne

na Mbili, Laki Tatu Tisini na Tatu Elfu na Sabini (Tshs.1,402,393.070); Hadi tarehe 31 Machi, 2022, Programu iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Saba na Sita, Laki Moja, Mia Moja Thalathini (Tshs.706,100,130) ambayo ni sawa na asilimia 50 ya makadirio.

## 4.2 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kila Mzanzibari anafanya Shughuli za Kiuchumi za Kumuwezesha Kumudu Mahitaji yake ya Msingi.

### 4.2.1 Programu ndogo SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**26. Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo ya (SA070301) ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina madhumuni ya kuwawezesha wananchi wenye kipato kidogo kupata mitaji ya kufanya shughuli za uzalishaji ili kujiajiri na kuinua vipato vyao. Walengwa wakuu wa mfuko ni vijana, wanawake, wahitimu wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Amali na Sekondari, Wastaafu na Watu walio katika makundi maalum. Programu ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina lengo la Kuimarisha Upatikanaji wa Mikopo Nafuu kwa Wananchi kwa kipindi cha mwaka 2021/2022,

Programu imetekeleza yafuatayo:-

1. Imefanya mapitio ya Miongozo ya kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo pamoja na mambo mengine imefanya mapitio na kuimarisha sekta ya Mitaji na Utoaji mikopo. Lengo likiwa ni kuwafikia wananchi wa makundi yote na kutoa huduma mwafaka za mitaji, mafunzo na masoko ili kuondoa manung'uniko yaliyokuwa yakitolewa na sehemu kubwa ya wananchi. Pia, Katika kufanikisha mchakato huo, Program ya Mfuko ilisitisha shughuli za utoaji wa mikopo kwa mwaka wote na ukawa unaendelea kuwapatia mafunzo na kufuatilia mikopo iliyokuwa mikononi mwa wananchi. Katika kipindi hicho, mikopo iliyokuwa inatolewa ni ya Mradi wa Mboga na Matunda tu ambao ulifadhiliwa na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) kupitia Program ya FEED THE FUTURE.

2. Kupitia Mradi huo wa Mboga na Matunda Mfuko umetoa mikopo Mia Mbili Thamanini na Sita (286) Unguja na Pemba yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Mbili Hamsini na Tatu, Laki Moja na Hamsini Elfu (Tzs. 253,150,000/=). Kati ya fedha hizo, Pemba imetolewa mikopo 162 yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja Thalathini na Tatu na Laki Tano (Tzs 133,500,000/=) na Unguja imetolewa mikopo 124 yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Tisa, Laki Sita na Hamsini Elfu (119,650,000/=).

3. Mikopo hiyo imetolewa kwa mkulima mmoja mmoja ambapo wakulima Mia Moja Sitini na Tano (165) wanawake na wakulima Mia Moja Ishirini na Moja (121) wanaume. Asilimia themanini na tisa (89%) ya waliopatiwa mikopo ni vijana kati ya miaka kumi na nane (18) hadi thelathini na tano (35). Wakulima hao 286 waliopatiwa mikopo waliweza kujiajiri wao wenyewe na kuwaajiri wananchi wengine 729 kufanya watu waliofaidika na shughuli za kiuchumi kufikia 1,015 kwa mwaka huo.

4. Mfuko katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 umefanikiwa kuongeza uwezo wake wa kukopesha baada ya kupata Mradi wa pili wa uendelezaji kilimo cha Mboga na Matunda wenye thamani ya shilingi Milioni Mia Moja (TZS 100,000,000/=) kutoka Mradi wa FEED THE FUTURE ikiwa ni sehemu ya mikakati ya Mfuko kutunisha fedha zake. Fedha hizo zote zimepatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2022. Kwa ujumla mradi wa Mboga na Matunda umemalizika rasmi tarehe 31 Disemba, 2021 na ulikuwa na thamani ya Shilingi Milioni Mia Nne na Hamsini (450,000,000/=) ambazo sasa zinatumiwa na Mfuko kutoa mikopo kwa Wananchi.

5. Vile vile, Mfuko kwa kushirikiana na Benki ya CRDB kupitia Mkopo wa fedha za IMF za Ahueni ya maradhi ya Uviko 19 umefanikiwa kuhakiki jumla ya vikundi 369 (Unguja 114 na Pemba

255) vyenye wanufaika 4,173 (Unguja 1,878 na Pemba 2,295) ambavyo vitapatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni Tatu na Milioni Kumi (3,010,000,000) (Unguja 1,107,500,000 na Pemba 1,902,500,000). Mikopo hii haina riba kwani Serikali ya Awamu ya Nane ya Dkt. Hussein Ali Mwinyi imeweka dhamana ya mikopo hii ili kuondosha usumbufu kwa Wananchi. Kazi ya kuratibu na kutoa mikopo hiyo inafanywa na Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji, Wizara ya Fedha na Mipango na Benki ya CRDB ambayo ndio itakayowapatia mikopo wajasiriamali. **Kiambatanisho nambari 3 (a) kinafafanua**

6. Mfuko umepata fedha za ziada kwa kuwekeza sehemu ya fedha zake katika Benki ya Biashara ya PBZ Ltd ambapo mfuko ulipata faida ya shilingi Milioni Thelathini na Nne (34,000,000/=) kutokana na kuwekeza Shilingi Milioni Mia Tano (500,000,000/=).

7. Mfuko umefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu na Ishirini na Saba Laki Nane Elfu Arobaini na Tisa na Mia Nne (327,849,400/=) Unguja na Pemba. Pemba imekusanya Shilingi Milioni Mia Moja na Thelathini na Nane, Elfu Sabini na Sita na Mia Moja (138,076,100/=) na Unguja imekusanya Shilingi Milioni Mia Moja Thamanini na Tisa, Laki Saba Sabini na Tatu Elfu na Mia Tatu (189,773,300/=). Marejesho haya ni wastani wa Shilingi Milioni Thelatini na Sita, Laki

Nne Ishirini na Saba Elfu, Mia Saba na Kumi na Mbili (36,427,712/=) kila mwezi, wakati mfuko umejipangia kukusanya Shilingi Milioni Arubaini (40,000,000/=) kwa mwezi na kushuka huku kwa marejesho kumechangiwa na maradhi ya Uviko 19 ambayo yamevuruga na kuathiri biashara nyingi za wajasiriamali wetu. **(Kiambatanisho nambari 3 (b) kinafafanua)**

8. Fedha zote zilizokopeshwa ni Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Kumi na Nne, Laki Tatu Sabini na Tatu Elfu (Tshs.5,314,373,000) ambapo zimerudishwa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tatu Kumi na Mbili, Laki Nne Sabini na Tano, Mia Moja Arubaini na Mbili Elfu (Tshs.3,512,475,142) na pesa ambayo ipo mikononi hadi Machi 31, 2022 ni Shilingi Mia Nane na Moja, Laki Nane Tisini na Saba, Mia tano Thamanini (Tshs.801,897,580).

9. Mfuko umewajengea uwezo wakopaji wote 286 katika masuala ya uandaaji mashamba, utunzaji wa mazao baada ya kuvunwa (Post harvest storage), taratibu bora za ukulima, lishe Bora, masoko na wakati gani wa kupanda na kuvuna. Pia wajasiriamali wengine waliendelea kupatiwa mafunzo juu ya uandaaji mpango wa biashara, usimamizi wa fedha, ujasiriamali na uwekaji wa mahesabu ya biashara zao. Kwa ujumla wajasiriamali 2,789) (wanawake: 1,597 na wanaume: 1,192 wamepatiwa mafunzo yaliyoelezwa ikiwa ni pamoja na kuwezeshwa kubuni miradi mipya.

27. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na taasisi za kifedha hususan mabenki, umejipangia kutoa mikopo elfu mbili (2,000) yenye thamani ya Shilingi Bilioni Tatu (3,000,000,000/=) kwa vikundi vya kiuchumi katika sekta zote za kiuchumi; Kuangalia fursa mpya za kiuchumi ambazo zinaweza kutekelezwa na wananchi katika sekta mbali mbali; Kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inatumiwa ipasavyo na inarudishwa kwa wakati uliopangwa; Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wateja wa mikopo kupitia data base; Kuendelea na juhudi mbalimbali za kutunisha fedha ili Mfuko uendelee kuwasaidia wajasiriamali wengi zaidi; Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa shughuli za mikopo nafuu hapa nchini; Kuimarisha mashirikiano na taasisi zinazotoa mikopo nafuu; Kuimarisha uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi; Kufanya Mapitio ya Muongozo wa Usimamizi wa Mikopo ili uende sambamba na mabadiliko ya Sera na Sheria mpya pamoja na kuimarisha uratibu na taasisi za fedha nchini.

28. **Mheshimiwa Spika**; Ili Program ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naliomba Baraza lako kuidhinisha ruzuku ya Shilingi Milioni Mia Tatu Ishirini, Laki Sita na Elfu Tano (Tshs.320,605,000) kwa ajili ya matumizi kazi za kawaida.

### 4.2.2 Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.

**29. Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo ya (SA070302) ina lengo la kusimamia Mageuzi ya Mfumo wa Vyama vya Ushirika ili viwe imara, endelevu, vinavyoendeshwa kiujasiriamali na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama, kiuchumi na kijamii. Pia, inachangia kukuza ajira na pato la Taifa. Programu hii inaendeshwa kupitia Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar inasimamia utekelezaji wa Sheria nambari 15 ya mwaka 2018. Programu ilitekeleza yafuatayo:-

1. Imesajili vyama vya ushirika 1,848 (Unguja 709 na Pemba 1,139), SACCOS 04 na vyama vya uzalishaji na utoaji wa huduma 910. Lengo ni kusajili vyama 201 (Unguja; 125, Pemba 76). Vyama hivi vinafanya kazi katika masuala ya Biashara ndogo ndogo, Utengenezaji Sabuni, Huduma za Vyakula Mashuleni, SACCOS, Ukataji miwa, Welding, Uvuvi, Ufugaji kaa, Kilimo, Ufugaji kuku, Usafi wa Mazingira, Wauza Vinyago, Ushoni, Kilimo cha Mwani, Ufundi wa vifaa vya Elektroniki, Upishi, Uchoraji, Uhifadhi wa koko. Zoezi hili limeongeza idadi ya vyama vilivyosajiliwa kufikia 5,950.

2. Imekagua hesabu za Vyama vya Ushirika 331 (Unguja 82 na Pemba 249) kwa kushirikiana na washirika. Lengo ni kukagua hesabu za

Vyama vya Ushirika 177 (Pemba 60 na Unguja 117). Matokeo yameonesha changamoto za mitaji midogo, utunzaji wa kumbukumbu hasa za hesabu na masuala ya utawala bora katika uendeshaji wa vyama unahitaji kuimarishwa. Changamoto hizi zinaendelea kufanyiwa kazi na Afisi.

3. Imefuatilia uendeshaji wa shughuli za vyama, utunzaji wa vitabu, ufuatwaji wa sheria katika vyama vya ushirika na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa vyama 769 Unguja na Pemba. Lengo ni kufuatilia vyama 484. Changamoto zilizobainika ni pamoja na vyama kutokufuata sheria ya ushirika, utunzaji wa kumbukumbu, taaluma ya ushirika, utunzaji wa taarifa za fedha za ushirika na mitaji midogo hasa katika vyama vya uzalishaji. Kutokana na changamoto hizo Afisi imejipanga kutoa taaluma ya ushirika katika maeneo ambayo vyama hivi vinahitaji. Aidha, jumla ya vyama 12 vimekata leseni.

4. Imetoa mafunzo juu ya Dhana ya Ushirika, Utaratibu wa usajili, Utunzaji wa kumbu kumbu, utunzaji wa miamala ya fedha kwenye madaftari, uhamasishaji wa kuongeza Hisa, Mpango kazi na Bajeti, Utayarishaji wa Masharti ya Ushirika, Mtiririko wa fedha, Mabadiliko ya Mtazamo, Ujasiriamali, Sheria ya Ushirika, Kazi na majukumu ya Viongozi, Elimu ya Uongozi, Utawala Bora, Faida na Umuhimu wa kujiunga na SACCOS kubwa na Matumizi ya Muda pamoja na

mafunzo ya Biashara. Jumla ya washiriki 6,979 (wanawake 4,383; wanaume 2,596) kutoka vyama 977 walipatiwa mafunzo hayo. Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha ufanisi wa utendaji wa vyama vya ushirika.

5. Imesimamia Mabaraza ya wanaushirika yenye lengo la kutatua changamoto zinazowakabili na kupeana taaluma ya ushirika kwa maendeleo ya vyama vya ushirika. Jumla ya Mabaraza 4 ya wanaushirika yamesimamiwa ambapo wanaushirika 46 (wanawake 22 na wanaume 24). Katika Mabaraza haya wanachama walipata fursa ya kujua umuhimu wa kuwa na Mikataba ya kazi, uhamasishaji juu ya vyama vya uzalishaji kujiunga na SACCOS ili waweze kuendeleza miradi yao. Aidha, SACCOS zote zilitakiwa kuzifanyia marekebisho Sheria zao Ndogo (By Law) ili ziende sambamba na Sheria na kanuni za Ushirika.

6. Iliadhimisha Siku ya Ushirika Duniani ambapo kilele chake kilifanyika tarehe 03/07/2021 katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdulwakil. Jumla ya washiriki 330 wakiwemo wajasiriamali 30 (Unguja 10 na Pemba 20) walipata fursa ya kushauriana na kubadilishana uzoefu wa jinsi ya kuimarisha vyama vyao, kupeana taaluma, kuonesha na kutafuta masoko ya bidhaa zao na kupata kujuana. Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Kwa Pamoja Tujenge Ushirika". Washiriki walikuwa ni wanaushirika na wajasiriamali kutoka

Mikoa yote ya Zanzibar, Maafisa Ushirika Unguja na Pemba, Vyama Vikuu vya Ushirika vikiwemo CUZA, ZASCCU, FARAJA UNION Ltd na Vyama Vikuu vya Mikoa.

7. Imeimarisha matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa za Vyama vya Ushirika. Taarifa za vyama 5,997 kati ya vyama 12,796 vilivyomo katika Daftari la Usajili zimeingizwa hii ni sawa na asilimia 94. Kati ya hivyo, vyama 3,042 vipo Unguja na 2,955 vipo Pemba.
8. Imetoa mafunzo juu ya Bima na umuhimu wake, mafunzo hayo yametolewa kwa kushirikiana na kampuni ya Bima ya Bumaco (BUMACO Insurance Company ltd) ambapo jumla ya wanachama 76 (wanawake 48 na wanaume 28) walinufaika na mafunzo hayo. Aidha, vyama vilipata fursa ya kujua aina mbali mbali za huduma za Bima ambazo zinatolewa na shirika hili. Pia, vyama vilipewa fursa ya kuwa wakala wa Bima katika kampuni hiyo. Mafunzo hayo yametolewa kwa Wilaya tano za Unguja.
9. Imeshiriki katika utatuzi wa migogoro kwenye vyama vya ushirika jumla ya migogoro kumi na moja (11) ilijitokeza kutoka vyama vya ushirika kwa kipindi hiki ambapo migogoro yote hii imetatuliwa, vyanzo vya migogoro hiyo ni wanachama kutaka kusajili ushirika ndani ya ushirika, mvutano baina ya wanachama na

Viongozi juu ya masuala ya Uwazi na uwajibikaji, Mikutano na uchaguzi, na baadhi ya watu kufanya biashara katika eneo lilokatazwa yaani Funguni, wanachama kudai haki zao, mwanachama kusimamishwa kazi, matumizi mabaya ya fedha za ushirika, kupatiwa uanachama na kupangiwa kazi na ruhusa ya kuuza namba za kazi za wanachama ili mwanachama aache ushirika. Migogoro hiyo imetatuliwa.

10. Imeshiriki katika kusimamia Mikutano ya vyama vya ushirika na jumla ya mikutano saba (7) ilisimamiwa kutoka katika vyama kumi (10) vya ushirika (UMAWA, Airport Taxi SACCOS, Tupendane, Makuli Multipurpose, Kusini Mpya SACCOS, Teacher's Development SACCOS, Dhowshed, Maendeleo, Tusisahau na Mtwango SACCOS) na vikundi kumi na nane (18) vya wilaya Mjini. Jumla ya wanachama 1,622 (wanawake 585 na wanaume 1037) walishiriki katika mikutano hiyo. Lengo la mikutano hiyo ni kuwasilisha ripoti za Ukaguzi za vyama vya Ushirika, Mikutano ya kufungua hesabu nyengine ya Benki kwa ajili ya malipo ya ZSTC na Mikutano Mikuu ya mwaka ya Ushirika pamoja na kuwafahamisha viongozi juu ya umuhimu wa uwekaji wa kumbukumbu na kuwakumbusha juu ya umuhimu wa utekelezaji wa majukumu yao na mgawanyiko wa majukumu, kuwafahamisha umuhimu wa Uchaguzi wa Viongozi wa Ushirika.

11. Imeviunganisha vyama 438 Vimejiunga na Kufungua Hesabu zao Benki (PBZ 146; Equity 9; CRDB 280; NMB 3) lengo ni kuhakikisha usalama wa fedha za wanachama. Pia, Programu imevitembelea vyama vya Tumwambie nini, Ulezi kazi, Vanilla Growing, Njaa ni tatizo, Ukindu Family, lengo ni kuangalia changamoto zinazowakabili wanaushirika hao hasa katika suala la upatikanaji wa masoko wa bidhaa, kufanya utafiti mdogo wa utoaji wa mikopo na urejeshaji.

12. Imefanya ziara mbili (2) katika Wilaya ya Kusini za kuvitembelea vyama vya Mtule Amcos Shehia ya Paje na Juhudi Zetu Shehia ya Bwejuu Dongwe kwa lengo la kuangalia maendeleo ya vyama na changamoto ambazo zinawakabili katika uendeshaji wa shughuli zo za kiushirika. Katika kutekeleza masuala ya mtambuka jumla ya wajasiriamali 5 (wanawake 3 na wanaume 2) wenye aina za ulemavu za uoni, viungo na ulemavu wa ngozi walipatiwa taaluma ya mwanzo na taaluma ya ujasiriamali katika vikundi/ushirika vitatu (3) ambavyo ni Kikundi cha wasioona (MUAMKO), Vijana wajasiriamali na Mambo Murua. Pia, Ilifanya ziara ya kutembelea SACCOS ya Donge Mtambile kwa lengo la kubadilishana mawazo na kujua juu ya upokeaji wa taarifa ya kuwekwa kwa jiwe la Msingi jengo lao katika shamra shamra za maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

30. **Mheshimiwa Spika**; Program kwa mwaka wa fedha 2022/23, imepanga kusajili vyama vya ushirika Mia nne (400); itakagua mahesabu ya vyama Mia tatu hamsini (350); itafanya ukaguzi wa kawaida kwa vyama Mia Nane (800); itatoa miongozo kwa vyama Elfu Tatu (3000) na itajenga uwezo wa kiutendaji wa vyama vya ushirika Elfu Tatu (3000).

31. **Mheshimiwa Spika**; Ili Program ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Milioni Mia Sita Thamanini na Saba, Laki Saba Sabini na Saba Elfu (Tshs.687,777,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 4.2.3 Programu Ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

32. **Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo (SA070303) hii ina lengo la kukuza Hadhi ya kiuchumi kwa vijana, wanawake, watu wazima na makundi maalum katika jamii na ina jukumu la kubuni na kuratibu Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuwawezesha wananchi kujiajiri na kuwa na kipato endelevu cha kuweza kumudu maisha yao. Msingi wa malengo haya ni kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi wao

na kuchangia katika kuleta maendeleo ya nchi. Programu ina vituo viwili ambavyo vinasaidia utekelezaji wa shughuli za Programu, Vituo hivyo ni Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali kiliopo Mbweni na Kituo cha Wanawake cha Kutengeneza Umeme wa Jua kilichopo Kinyasini. Programu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imetoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wajasiriamali wanaotengeneza sabuni za aina mbali mbali pamoja na utafutaji wa masoko mtandaoni (E- marketing), jinsi ya kutengeneza bidhaa bora na kuzitangaza. Mafunzo haya yaliwashirikisha wajasiriamali Mia Moja (100) (74 wanwake na 26 wanaume) kutoka katika Wilaya zote za Unguja. Vile vile, ilitoa mafunzo ya Ujasiriamali kwa wajasiriamali Mia Mbili Ishirini na Moja (221) (169 wanawake, 50 wanaume) kutoka katika Wilaya zote za Pemba.

2. Imevitembelea na kuvikagua vikundi mbali mbali vya Wajasiriamali Unguja na Pemba ili kupatiwa ushauri wa kuviimarisha vikundi vyao na uzalishaji. Jumla ya vikundi vya wajasiriamali arubaini na nne (44) vimetembelewa Unguja na Pemba vikundi 53. Pamoja na kufanya tathmini/ uhakiki wa vikundi kupitia Programu ya Fedha za IMF ya maradhi za UVIKO 19 katika Mikoa 3 ya Unguja ambapo vikundi Mia Moja Sitini (160) vilihakikiwa (Kaskazini 27, Kusini 38 na Mjini 95).

3. Kwa kushirikiana na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeweza kushiriki katika Maonesho ya Afrika Mashariki maarufu kama Jua Kali Nguvu Kazi pamoja na kuwasaidia nauli wajasiriamali Arubaini na Sita (46) (35 wanawake, 11 wanaume) kuweza kushiriki katika maonesho hayo. Maonesho hayo yameimarisha ushiriki wa wajasiriamali na wafanyabiashara wa Zanzibar, wamebadilishana uzoefu na kukuza mbinu za uzalishaji pamoja na kukuza masoko ya biashara.

4. Imeanza kutoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki kwa wajasiriamali 200 (Kusini Unguja 50, Kaskazini Unguja 50, Kaskazini Pemba 50 na Kusini Pemba) kupitia Program ya Uwezeshaji ya fedha za IMF za Ahueni ya Uviko 19. Mafunzo haya yanatarajiwa kutolewa kwa Wajasiriamali 750 (Unguja 400 na Pemba 350). Wajasiriamali hawa wakimaliza mafunzo wanapatiwa vifaa vya ufugaji wa nyuki na kila mmoja anatarajiwa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 4 ambapo mradi huu unatarajiwa kuwanufaisha wajasiriamali 3,000.

5. Imesimamia uendeshaji wa Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali (ZTBI) ambapo wajasiriamali Tisini na Sita (96) wanawake wameweza kushiriki katika mafunzo ya ujasiriamali kupitia mradi wa Youth Challenge International (YCI). Na wajasiriamali Sitini na Tatu (63) (47 wanawake, 16 wanaume) wamepatiwa mafunzo

ya usimamizi wa fedha, masoko na kufahamu masharti ya kusajiliwa katika Bodi ya Chakula na Madawa (ZFDA) ambao tayari walishaingia katika mradi wa Feed The Future.

6. Kupitia Kituo Cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali (ZTBI) imefanya mafunzo ya ubunifu (innovation) kwa watendaji wa Kituo hicho kwa ajili ya kuwajengea uwezo watendaji hao. Mafunzo hayo yanalengo la kuwawezesha watendaji kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kuimarisha utoaji wa huduma za kituo hicho. Baada ya mafunzo hayo watendaji hao wameshauriwa kutengeneza Mpango Mkakati utakaojumuisha shughuli na mikakati maalum ya kukiimarisha Kituo hicho.

7. Kupitia Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali, imerasimisha (usajili) biashara za wajasiriamali katika Ofisi ya BPRA. Hivyo, vikundi Kumi na Moja (11) kati ya Kumi na Tano (15) vimeweza kusajili kampuni zao kwa ajili ya kuendeleza biashara zao. **Kiambatanisho nambari 4 kinahusika**

8. Katika kuhakikisha wajasiriamali wanaelewa shughuli zinazofanywa na Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali ZTBI, Programu imefanya matangazo ya kukitangaza kituo hicho na shughuli zake katika radio, televisheni ya ZBC na tovuti ya kituo ili kutangaza shughuli za Kituo.

9. Vile vile, Programu imesimamia uendeshaji wa Kituo cha Wanawake cha Utengenezaji wa Vifaa vya Umeme wa Jua (Barefoot College) ambapo ununuzi wa umeme, mashine ya kisima na matengenezo yalifanywa ili kuimarisha upatikanaji wa maji kituoni.

10. Imefanya ziara za ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya mradi wa umeme wa jua. Jumla ya nyumba Mia Moja Tisini na Nane (198) zilizounganishwa na umeme wa jua zimekaguliwa na kufanyiwa marekebisho ya vifaa kwa Unguja na Pemba vilivyokuwa vina khitilafu. Pia, wanakijiji wametaka uwezo wa sola uongezke ili waweze kutumia vifaa hivyo. Pia, ilifanya ziara katika kijiji cha Makoongwe kutathmini maendeleo ya Mradi wa Nishati ya Solar wanayotumia wanakijiji.

11. Kwa upande wa mradi wa nyuki ziara za kukagua mradi huo zilifanyika katika vijiji mbali mbali vya Unguja na Pemba pamoja na kijiji cha Tarakea, Moshi. Lengo la ukaguzi huo ni kuangalia maendeleo ya miradi ya nyuki baada ya kuwapa mafunzo; kuangalia kinamama waliopewa mafunzo ya uwezeshaji namna wanavyoyafanyia kazi mafunzo hayo ambapo kwa upande wa Tarakia Moshi mama 2 wameweza kuzalisha lita 20 za asali kwa miezi 3.

12. Imeendelea na utaratibu wa utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali Mia Mbili Sitini na

Nane (268) (114 wanawake na 154 wanaume). Mafunzo hayo ni miongioni mwa program za uviko 19 za kuwawezesha Wananchi kiuchumi.

**33. Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2022 – 2023, Programu ya Uratibu na Uendelezaji wa Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imejipanga Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kuandaa Mpango wa Mafunzo ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara ambao utaendana na mahitaji ya mafunzo na soko la bidhaa za wajasiriamali; Kuimarisha Miundombinu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa Programu mbalimbali za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kuimarisha upatikanaji wa Takwimu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; kuandaa Muongozo wa kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Miradi ya kimkakati na miradi ya ZIPA (local content) na Kufanya tafiti zinazohusiana na shughuli za Wakala

**34. Mheshimiwa Spika**; Vile vile, Program imejipanga kuendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 624, wanawake na makundi maalum; itatekeleza miradi ya kuwawezesha wajasiriamali na vijana ili kutoa huduma na bidhaa zenye ubora; itawawezesha wajasiriamali mia mbili (200) kushiriki katika maonesho ya Afrika Mashariki (Jua Kali); itaendelea kuwawezesha Vijana kujiajiri kupitia Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali (ZTBI) pamoja na kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia Kituo cha

Wanawake cha utengenezaji wa vifaa vya umeme wa jua (Barefoot) Kibokwa na itaanya ufuatiliaji wa nyumba 250 zilizounganishwa umeme wa jua.

**35.** **Mheshimiwa Spika**; Ili Programu ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Program za Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022 – 2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni Ishirini na Nane, Milioni Mia Tatu Sitini na Tisa, Laki Tatu Ishirini na Tano Elfu (Tshs.28,369,325,000) kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo.

**36.** **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu **(PA0703)** ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kipindi cha Julai – Machi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Ishirini na Tisa, Laki Nane Arubaini na Tano Elfu, Mia Tisa Sabini na Saba (Tshs.1,729,845,977); Hadi tarehe 31 Machi, 2022, Programu iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Saba Hamsini na Tisa, Laki Nne Thamanini na Mbili, Mia Tisa Thalathini na Sita (Tshs.759,482,936) ambayo ni sawa na asilimia 44 ya makadirio.

## 4.3 PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI.

**Matokeo ya muda Mrefu**: Kuwa na Sheria, Sera, Programu, Tafiti na Mipango Endelevu itakayoimarisha Uratibu, Uandaaji na Utekelezaji wa Sheria za Kazi, Upatikanaji wa Ajira za Staha na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 4.3.1 Programu ndogo SA070501: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi

**37. Mheshimiwa Spika**; Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi inalenga kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Sera, Mipango, Programu na Tafiti za Afisi ili kuimarisha upatikanaji wa Ajira zenye Staha, Sheria na Viwango vya Kazi pamoja na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Programu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imeandaa Agenda za Utafiti za Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji na kufanya mafunzo ya utafiti kwa watendaji wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Kupitia mafunzo hayo, Afisi imeweza kuibua maeneo mbali mbali ya kipaumbele ya kufanyiwa tafiti kwa muda wa miaka mitano ijayo kwa mujibu wa majukumu ya Afisi. Agenda ya utafiti tayari imeshajadiliwa

katika kikao cha Kamati tendaji na tayari kwa kutumika. Vile vile, kupitia Agenda hiyo imeandaa Maeneo ya kufanyiwa tafiti na gharama zake kwa mujibu wa maeneo na majukumu ya Afisi.

2. Imeandaa Nyenzo za kukusanya takwimu (Viashiria) za Afisi kwa kutumia viashiria vya Dira 2050, SDGs na Agenda 2063 ili kuweza kukusanya takwimu za Afisi kwa ufanisi.

3. Imekamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Afisi (2022-2027) kwa kushirikiana na Tume ya Mipango na iko tayari kwa kujadiliwa na Kamati ya Uongozi ili kupata maoni na zitaanza kutumika rasmi kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023.

4. Imenunua samani ya vitengo vya Idara ya Mipango Sera na Utafiti ili kuimarisha mazingira ya kiutendaji. Samani zilizonunuliwa ni pamoja na meza 3, viti 3 na kabati la kuhifadhia nyaraka, computer na UPS. Vile vile, Programu imefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali kwa ajili kuimarisha kitengo cha Habari na Mawasiliano ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na computer ya intel core 7, Access point, flash na tool box vimenunuliwa.

5. Imeandaa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inayoendana na mahitaji ya sasa ikiwemo kuingiza maeneo mapya yanayoibua fursa zinazohitajika, ikiwemo masuala ya mafuta na gesi pamoja na Uchumi wa Buluu. Pia, imeratibu

uandaaji wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Muongozo wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Sera, Sheria na Muongozo huo vitasimamia utekelezaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao utakuwa ni mratibu mkuu wa masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na shughuli zote za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi nchini.

6. Inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Ajira 2009 kwa ajili ya kuandaa Sera mpya ya Ajira 2022 ambapo imeanza na hatua ya kuifanyia tathmini Sera yenyewe ili tahmini hiyo iweze kutumika katika mchakato wa uandaajia wa Sera mpya. Tathmini inaonesha kwamba kuna haja ya Sera hiyo kufanyiwa mapitio kutokana na mabadiliko mbali mbali yanayotokea nchini ikiwemo uwepo wa Dira 2050, Ilani ya Uchaguzi 2020 - 2025 na mabadiliko ya kidunia. Pia, mchakato wa mapitio ya Sheria ya Ajira yanahamasisha mapitio ya haraka ya Sera hii.

7. Imeandaa na kuwasilisha maandiko ya miradi Tume ya Mipango inayogharamiwa na fedha za IMF za Ahueni ya Maradhi ya Uviko 19 inayosimamia masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo inaratibiwa na Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ili kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Pia, inaendelea kuratibu mchakato wa utekelezaji wa miradi

inayofadhiliwa na fedha za IMF za Ahueni ya Maradhi ya Uviko 19 ambapo jumla ya Miradi mitano (5) inatekelezwa chini ya Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo kwa pamoja inagharimu jumla ya Shilingi Bilioni Thamanini na Moja, Milioni Mia Nane Sitini na Sita, Laki Moja Hamsini na Nane, mia Tisa na Kumi (81,866,158,910). Miradi hiyo ni pamoja na :-

i. Mradi wa Kuimarisha Sekta ya Uvuvi ili kuongeza Ajira (Uchumi Buluu);
ii. Mradi wa Kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
iii. Mradi wa Ujenzi wa Maeneo ya Kufanyia Biashara Unguja na Pemba (Mbao, Vyuma na Garage);
iv. Mradi wa Kuwawezesha Vijana na Wanawake katika Ufugaji wa Nyuki; na
v. Mradi wa kuwawezesha Vijana wanaoacha Madawa ya Kulevya.

Kati ya miradi hii miradi miwili nambari i na iv ndio inayosimamiwa utekelezaji wake na Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambayo kwa pamoja inagharimu jumla ya Shilingi Bilioni Thalathini na Tatu, Milioni Mia Tisa Arobaini na Sita, Laki Mbili Ishirini Elfu (Tshs. 33,946,220,000).

8. Imeratibu na kusimamia zoezi la uhakiki wa vikundi vya wajasiriamali katika Mikoa 5 ya Unguja na Pemba kwa ajili ya kupatiwa mikopo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia fedha za IMF za Ahueni ya Maradhi ya Uviko 19. Zoezi la uhakiki limekamilika kwa hatua za awali na jumla ya vikundi Elfu Tatu Mia Nne na Tisiini na Nne (3,494) vimehakikiwa; kati ya hivyo Elfu Mbili Mia Tisa na Saba (2,907) vinaweza kuendelea na mchakato, na Mia Tano Themanini na Saba (587) vinahitaji kuimarishwa ili viweze kukopesheka. Kati ya Vikundi Elfu Tatu Mia Nne Tisini na Nne (3,494); vikundi Mia Tisa Thelathini na Tatu (933) ni vya Uchumi wa Buluu na Elfu Mbili Mia Tano Sitini na Moja (2,561) ni vya Uwezeshaji. Afisi inaendelea kushirikiana na Serikali za Mikoa na Wilaya kupokea maombi ya vikundi na Mikopo imeanza kutolewa Unguja na Pemba.

9. Imefanya mafunzo ya Uandishi wa Miradi na Maandiko ya Miradi kwa Watendaji 35 Unguja na Pemba ili kuimarisha ufanisi wa Kazi. Watendaji hao wameandaa Maandiko 2 ya miradi ambayo yatasambazwa kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutafuta fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.

10. Inaendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi na kuwasilisha changamoto zinazojitokeza katika taasisi husika ili waweze kuzifanyia kazi. Maeneo yaliyofanyiwa ufuatiliaji

ni pamoja na Wakala Binafsi wa Ajira, Zanzibar Beach Resort Hotel, Zainab Bottlers Company Ltd, Skuli ya Mtopepo, Basra Textile Mills Ltd na Nyumba zilizofungiwa Umeme wa Jua katika Vijiji vya Makunduchi na Mtende. Pia, ufuatiliaji ulifanywa katika Kituo cha Huduma za Ushauri wa Kibiashara Wilaya ya Kaskazini A, Kaskazini B, Kusini na Kati. Vile vile, ilitembelea vikundi vilivyonufaika na Mikopo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Mkoa wa Mjini Magharibi na vikundi vya Ushirika vilivopewa mafunzo Matarumbeta. Vile vile, ziara za ufuatiliaji zimefanywa Pemba kuangalia utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Afisi. Lengo la tathmini ni kubaini changamoto na kuweza kuzifanyia kazi.

11. Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji ikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 - 2025 na ripoti maalum zilizohitajika kwa vipindi tofauti zinazohusiana na utekelezaji wa shughuli za Afisi katika taasisi mbali mbali.

12. Imelipia gharama za safari za ndani ya nchi kwa wafanyakazi ili kushiriki katika vikao na shughuli mbali mbali za Afisi zinazohusiana na masuala ya Kazi na Uwezeshaji.

13. Inaendelea kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari (Redio, Televisheni, Magazeti, Facebook, Twitter na Tovuti ya Afisi) mbali mbali nchini kuhusiana na utekelezaji wa shughuli za Afisi, jumla

ya vipindi Kumi na Tatu (13) na Habari Arubaini (40) vimerushwa hewani kupitia Televisheni na Redio; Makala tano (5) zimeandaliwa na Kijarida cha Afisi cha kutimiza mwaka 1 wa utekelezaji shughuli za Afisa kimeandaliwa.

14. Inaendelea kuratibu na kusimamia ujenzi wa vituo vya kuchakata mazao yanayotokana na nyuki Kizimbani Unguja na Pujini Pemba ambavyo pamoja na mambo mengine vitatumika kuzalisha bidhaa za nyuki, kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki, kusimamia ubora wa bidhaa za mazao ya nyuki ikiwemo mnyororo wa thamani. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu tokea kuanza kwake.

15. Imefanya ziara ya Mashirikiano baina ya ARKUU na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi la Tanzania Bara kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na kujifunza namna bora ya kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar. Katika ziara hiyo, Watendaji walijifunza namna ya uendeshaji wa Baraza la Uwezeshaji wananchi kiuchumi ikiwemo Mifuko ya Uwezeshaji, kuendesha majukwaa ya uwezeshaji ya wanawake, Madawati ya Wanawake na Program mbali mbali za kuwawezesha wananchi kiuchumi. Pia, Watendaji walijifunza masuala ya mageuzi ya vyama vya ushirika kwa maendeleo ya jamii na nchi kwa ujumla.

38. **Mheshimiwa Spika**; Program kwa mwaka wa fedha 2022/23, imepanga kuendelea na mapitio ya Sera ya Ajira na Sera ya Maendeleo ya Ushirika; Kutoa kopi za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kufanya tafiti 3 kwa mujibu wa Agenda za Utafiti; Kuandaa Kanuni za Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Afisi; Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi; Kuratibu Mfumo wa TEHAMA na upatikanaji wa habari na taarifa za Afisi; Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

39. **Mheshimiwa Spika**; Ili Program ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita Hamsini na Nane, Laki Nne na Elfu Tatu (Tshs.658,403,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 4.3.2 Programu Ndogo SA070502: Utawala na Uendeshaji.

40. **Mheshimiwa Spika**; Programu ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Uendeshaji na Utumishi za na kukuza uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Programu kwa mwaka wa fedha

2021/2922, imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imesimamia malipo ya Safari za ndani Kumi na Tatu (13) za viongozi na Watendaji wa Afisi kwenda Pemba, Dar es salaam, Dodoma na Mwanza, imefanya matengenezo ya gari sita (6), imelipia bima gari mbili (2) na kusimamia ununuzi wa mafuta kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali. Pia, inaendelea kugharamia malipo ya Umeme, gharama za Ulinzi, kugharamia washiriki wa Maonyesho ya sherehe za Mapinduzi Pamoja na ununuzi wa gari moja (1).

2. Imesimamia ununuzi wa vifaa vya kuandikia, samani za Afisi, vitendea kazi kwa lengo la kumarisha utendaji kazi. Vile vile, inatarajia kufanya ukarabati wa ukumbi wa mkutano pamoja na Afisi nyenginezo kwa kuwekea samani na vitendea kazi vipya.

3. Imesimamia ulipaji wa posho za likizo kwa wafanyakazi Hamsini na Tisa (59), malipo ya saa za ziada kwa wafanyakazi Kumi na Mbili (12) malipo ya ufiwa kwa wafanyakazi wanane (8), posho la simu kila mwezi kwa watendaji kwa shughuli za ufuatiliaji, imesimamia mafunzo mafupi kwa watendaji Hamsini na Nne (54), imelipia mafunzo ya awali kwa wafanyakazi

Ishirini na Saba (27) pamoja na kulipa posho la kujikimu kwa wafanyakazi Ishirini na Saba (27) waliopatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Utawala wa Umma (IPA). Aidha, programu inaendelea kuwalipia ada wafanyakazi wawili (2) waliopo katika mafunzo ya muda mrefu. Na imefuatilia malipo ya kiinua mgongo kwa wastaafu sita (6).

4. Imefanya upimaji utendaji kazi (Performance Appraisal) kwa wafanyakazi hamsini na moja (51) ambao tayari wameshapatiwa nyongeza ya mshahara ya mwaka.

5. Imefanya uhakiki wa Wafanyakazi na vitendea kazi kwa ajili ya kufahamu changamoto, mapungufu na mahitaji yaliyopo ili kuweza kuangalia namna bora ya kuimarisha ufanisi wa Afisi pamoja na kufanyika kwa uhamisho wa ndani. Tayari uhamisho wa ndani umefanyika kwa baadhi ya Wafanyakazi kwa kuzingatia elimu na uzoefu ili kuongeza ufanisi katika kazi.

**41. Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Program ya Utawala na Uendeshaji itaendelea kusimamia Maslahi ya Wafanyakazi kama vile malipo ya mishahara, posho la likizo, malipo ya saa za ziada, malipo ya ubani kwa wafiwa pamoja na kuandaa na kufuatilia malipo ya viinua mgongo kwa

Wastaafu wetu; itaendelea kutoa mafunzo ya ndani, zoezi la Upimaji Utendaji kazi kwa Wafanyakazi kwa kila mwaka, kuimarisha mazingira ya Afisi nje na ndani; itaandaa Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimali watu; itasimamia ununuzi wa Genereta la Dharura, pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za kila siku.

**42. Mheshimiwa Spika,** ili program ndogo ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Sabini na Tatu, Laki Tatu Kumi na Tatu Elfu (Tshs.1,773,313,000) kwa kazi za kawaida na mishahara.

### 4.3.3 Programu Ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.

**43. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu imetekeleza yafuatayo:-

1. Imesimamia vyema maslahi ya wafanyakazi kwa kulipa fedha za likizo kwa watendaji kumi na mbili (12) (Wanawake wanne (4) na Wanaume

nane (8) na kulipa posho la masaa ya ziada kwa wafanyakazi ishirini na tano (25) wa kada ya udereva na ulinzi ambao wote ni wanaume na kulipia huduma ya mazishi kwa mfanyakazi mmoja (1). Pia, imelipia gharama za safari arubaini na mbili (42) za ndani ya nchi kwa wafanyakazi ili kushiriki katika vikao na shughuli mbali mbali za Wizara Unguja na Tanzania Bara. Pia, Afisi imemjengea uwezo mfanya kazi wake mmoja (1) wa kiume kwa kumpatia viza kwa ajili ya kuenda nje ya nchi kujiendeleza na masomo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (Phd).

2. Imefanya manunuzi ya kompyuta moja (1), magazeti ya kila siku pamoja na kulipia gharama za umeme, maji, simu, mafuta, vifaa vya usafi, vifaa vya kuandikia pamoja na huduma za mtandao. Pia, imelipia bima na gharama za matengenezo ya gari tatu (3) na ukarabati wa vifaa vya Afisi vikemo Vipooza hewa na mifereji pamoja na kufanya malipo ya huduma za usafi kwa kampuni inayotoa huduma za usafi Afisini.

3. Imefanya ufuatiliaji na tathmini kwa dhumuni la kuboresha utendaji wa shughuli mbali mbali za Afisi. Pia, imetayarisha ripoti za ufuatiliaji na tathmini kwa Idara mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kutatua changamoto zilizojitokeza. Ufuatiliaji huo ulifanyika kwa mradi wa umeme wa jua wa Bare foot Makoongwe, vyama vya

ushirika wanufaika wa mikopo kutoka Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na mradi wa ujenzi wa Kituo cha Kuchakata Asali kilichopo Limanda Pujini, Wilaya ya Chake- Chake.

4. Kwa upande wa mradi wa umeme wa jua Makoongwe, unakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wanufaika wa mradi huo kutolipa ada ya huduma wanayoipata. Changamoto hii imepelekea mradi kuwa na deni la malipo ya mafundi ambao ni wanamama watatu (3) waliopatiwa mafuzo ya uhandisi wa umeme wa jua kutoka Chuo cha Bare Foot College. Wanamama hao ndio wanaotoa huduma za ufungaji wa 'solar panel' kwa wataka huduma pamoja na kuzitengeza pale inapotokea hitilafu. Pia, mradi unakabiliwa na changamoto ya deni la posho kwa kamati ya kijiji inayosimamia mradi huo na ukosefu wa taaluma ya uwekaji wa kumbukumbu za kifedha. Pamoja na changamoto hizo, maoni ya wananchi wa Makoongwe wanahitaji mradi uendelee na unawasaidia sana hasa kwa wale wasiokuwa na umeme wa ZECO kwani umeme wa jua unawapunguzia gharama za matumizi ya mafuta ya taa.

5. Ufuatiliaji na tathmini iliyofanywa na Afisi unaonesha kwamba vikundi pamoja na wanufaika wa mikopo wanaendelea na shughuli zao vizuri. Aidha, baadhi ya vikundi vinakabiliwa

na changamoto ya elimu ya uwekaji wa kumbukumbu na ujasiriamali. Pia, baadhi ya wakulima wanakabiliwa na changamoto ya wadudu wanaoshambulia mazao yao. Afisi kupitia programu ya Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi imejitahidi kutoa taaluma ya uwekaji wa kumbukumbu na ujasiriamali kwa wanaushirika katika shehia mbalimbali Kisiwani Pemba. Kwa vikundi vya kilimo, Afisi ameshirikiana na wataalamu kutoka Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji kwa lengo la kutoa ushauri elekezi juu ya namna bora ya kuendeleza shughuli zao za kilimo na kupata mazao yenye tija.

6. Imefanya Uhakiki wa vyama vya ushirika Mia Tatu na Arobaini na Nne (344) kwa lengo la kupatiwa mkopo kupitia fedha zilitolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kupunguza athari za UVIKO 19 katika uchumi. Kati ya vikundi hivyo Afisi imefanikiwa kuwasilisha Benki ya CRDB vyama vya ushirika Mia Mbili na Sabini na Nne (274) kwa ajili ya kupatiwa mkopo wenye thamani ya shingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano na Tisini na Nane na Elfu Ishirini na Saba (2,598,027,000/-).

7. Kwa upande wa Kituo cha Kuchakata Asali kilichopo Limanda Pujini, Wilaya ya Chake-Chake shughuli za ujenzi zinaendelea vizuri na miundombinu ya maji imekamilika.

8. Imeratibu vikao vya kujadili rasimu ya sera na sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na kujadili muongozo wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mapendekezo mbali mbali yalitolewa na kuwasilishwa katika kikao maalum kilichofanyika Ofisi kuu Unguja. Kadhalika, imeratibu vikao vya kujadili shughuli mbalimbali za Afisi zitakazotekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 kwa mujibu vipaombele vya taifa ambavyo ni ilani ya uchaguzi ya CCM, Dira ya Maendeleo ya 2050 na maagizo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mapendekezo mbali mbali yalitolewa na kuwasilishwa katika vikao hivyo na kufanikiwa kuandaa bajeti inayozingatia vipaombele vya taifa. Kadhalika, Afisi imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji ikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM 2020 - 2025 na ripoti maalum zilizohitajika kwa mwaka wa fedha 2021/22

**44.** **Mheshimiwa Spika**; Program kwa mwaka wa fedha 2022/23 inaendelea na kusimamia maslahi ya wafanyakazi, utoaji wa mafunzo, kuratibu utekelezaji wa sera na sheria mbalimbali, kuandaa taarifa za utekelezaji na kufanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini za Afisi pamoja na kuripoti utekelezaji wake.

45. **Mheshimiwa Spika**; Ili Program ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Thalathini na Mbili, Laki Moja Tisini na Saba Elfu (Tshs.1,532,197,000) kwa ajili ya matumizi kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

46. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu **(PA0705)** ya Utumishi na Uendeshaji wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kipindi cha Julai – Machi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Moja Sitini na Saba, Laki Mbili Ishirini na Saba Elfu, Mia Tisa Sabini na Nane (Tshs.4,167,227,978); Hadi tarehe 31 Machi, 2022, Programu iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja Kumi na Moja, Laki Nne Elfu Kumi na Mia Tisa (Tshs.3,111,410,900) ambayo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio.

## 5.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## 5.1 PROGRAMU KUU: PA0801 KUIMARISHA UWEKEZAJI NA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI

**Matokeo ya muda mrefu:** Usimamizi na Ushajihishaji wa Mali za Umma kwa kuziweka katika Mfumo wa Mashirikiano kwa wote.

### 5.1.1 Programu ndogo SA080101: Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

47. **Mheshimiwa Spika**; Program ya Kuimarisha Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ina lengo la Kukuza, kuratibu na kuimarisha Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika sekta za kiuchumi na kijamii pamoja na kutekeleza miradi mbali mbali ya Maendeleo. Programu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imetekeleza shughuli zifuatazo:-

    1. Imepitia na kuchambua maombi ya miradi iliyowasilishwa na wawekezaji binafsi. Kwa kipindi cha miezi tisa (9) Kampuni Mia Moja Kumi na Sita (116) kutoka ndani na nje ya nchi ziliwasilisha maombi ya miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa PPP. Kati ya maombi hayo asilimia 41 ni ya sekta ya Miundombinu, asilimia 35 sekta ya

Nishati, asilimia 9 sekta ya Afya, asilimia 6 sekta ya Uchumi Buluu, asilimia 5 sekta ya huduma za kijamii, asilimia 3 sekta ya Kilimo na asilimia 1 Sekta ya Elimu.

2. Imefanya mapitio ya maombi Kumi na Tano (15) ya Kampuni zilizowasilisha maombi na kuyawasilisha katika Kamati ya Majadiliano (GNT) kwa kufanyiwa uchambuzi. Kampuni zilizokuwa hazikuwasilisha maombi ya miradi (Project Proposals) ni Makampuni yaliyowakilishwa na mawakala/madalali (Agents) wa miradi hiyo. Pia, inaendelea na mazungumzo na uchambuzi wa kitaalam kwa mradi wa Nyumba ya Kitalii (Domino), Kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki-Beit el ras na Mradi wa Kituo cha Mikutano na Biashara.

3. Imefanya marekebisho ya baadhi ya vifungu vya Kanuni ya PPP ili iendane na marekebisho ya Sheria ya PPP. Marekebisho ya vifungu hivyo yamefanyika na yamewasilishwa katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa msaada wa kisheria.

4. Imeandaa nyaraka za manunuzi za miradi na mikataba ya PPP. Nyaraka hizi za miradi zinazoandaliwa zitatumika kwa miradi itakayoibuliwa na kutekelezwa kwa mfumo wa PPP. Vile vile, Program kwa kushiriana na Benki ya Dunia iliwajengea uwezo watendaji wa Idara na Taasisi zenye miradi ya PPP katika Uchambuzi,

Mapatano (Negotiation) na Utayarishaji wa Mikataba.

48. **Mheshimiwa Spika**; Program Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa mwaka wa fedha 2022/23 imepanga kuibua, kuandaa miradi ya PPP; kuimarisha tovuti ya PPP; Kushiriki mijadala na maonesho yanayohusu miradi ya PPP ndani na nje ya nchi; Kujenga uwezo watendaji wa PPP na Sekta zenye miradi ya PPP; Kuratibu na kuwasilisha miradi kwa wadau na Ununuzi wa vifaa vya Ofisi.

49. **Mheshimiwa Spika**; Ili Programu Ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Mia Tatu Thamanini na Nne Elfu (Tzs.478,384,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

### 5.1.2 Programu ndogo SA080102: Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji.

50. **Mheshimiwa Spika**; Programu ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji ina lengo la kushajiisha Uwekezaji ndani na Nje ya Nchi na inatekelezwa na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar. Pia, ina lengo la kuweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na uimarishaji wa huduma mbali mbali

zitakazoimarisha Uwekezaji Nchini. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022, Programu imetekeleza yafuatayo:-

1. Imeidhinisha miradi Elfu Moja Mia Moja na Sabini na Tatu (1,173) tokea kuanzishwa kwake ambapo Miradi Mia Tatu Kumi na Moja (311) imefutwa na Miradi Mia Nane Sitini na Mbili (862) iko hai. Kati ya Miradi Mia Nane Sitini na Mbili (862), Miradi Mia Tatu Sabini (370) inatoa huduma, Miradi Sitini na Moja (61) iko katika hatua ya ujenzi na Miradi Mia Nne Thelathini na Moja (431) iko katika hatua mbali mbali za utekelezaji ambayo kwa ujumla ina mtaji wa makisio wa Dola za Kimarekani Bilioni Nane Nukta Moja Tano (Bilioni 8.15) zenye makisio ya kuzalisha ajira Sitini na Tatu Elfu Mia Nne Sitini na Mbili (63,462). Kati ya miradi yote iliyoidhinishwa, Sekta ya Utalii ina Miradi Mia Nne Hamsini na Sita (456) ambayo ni sawa na asilimia Hamsini na Tatu (53%) ya Miradi yote na inayotarajia kuzalisha ajira Thelathini na Moja Elfu Mia Mbili na Hamsini na Moja (31,251).

2. Pia, imeidhinisha jumla ya Miradi Sitini na Mbili (62) yenye mtaji wa makisio ya Dola za Kimarekani Milioni Mia Nne Arubaini na Tisa nukta Zero Nane (milioni 449.08) inayotarajiwa kuzalisha ajira Elfu Nne Mia Nne Sabiini na Tisa (4,479) kwa wazawa. Kati ya miradi hiyo mradi 1 uko katika hatua ya ujenzi na Miradi Arubaini na Saba (47) iko katika hatua za awali za uwekezaji.

3. Imeshiriki mikutano ya Kimataifa: Dubai, Italia na Rwanda. Vile vile, imeandaa Kongamano la Big BreakFast – Safari ya Ahuweni, Kongamano la Kimataifa la Uwekezaji katika kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika na Kongamano la Uwekezaji kati ya Tanzania na Uingereza. Pia, imepata fursa ya kushiriki "Namibia Promotion Day" iliyofanyika katika Ubalozi wa Namibia, Dar es salaam. Program hiyo ilikuwa na lengo la kuangalia fursa za uwekezaji zilizopo nchini Namibia. Mikutano na Kongamano hilo lilikuwa na lengo la kuitangaza Zanzibar katika masuala ya Uwekezaji.

4. Imepokea ugeni wa kidiplomasia kutoka Ubalozi wa Rwanda nchini Tanzania na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mh. Balozi Liberata MulaMula na Balozi wa Qatar nchini Tanzania ambapo Mamlaka iliweza kutumia fursa hizo kutangaza fursa mbali mbali za uwekezaji nchini.

5. Katika kuratibu na Kukuza mashirikiano ya kisekta, Programu imeandaa mikutano ya ushirikiano ya kisekta na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman na Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC). Kufuatia mikutano hiyo, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar imetia saini Hati ya Maelewano na Tanzania Investment Cooperation pamoja na kutia saini Mkataba wa "Non disclosure

Agreement (NDA)" na Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman.

6. Imetoa vibali Ishirini na Saba (27) vya ujenzi kwa miradi iliyosajiliwa na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar. Aidha, jumla ya vibali Mia Mbili Sitini na Mbili (262) vya kazi na vibali Mia Moja Themanini na Moja (181) vya ukaazi vimetolewa. Aidha, Program inaendelea na kazi ya kufanya marekebisho Sheria ya ZIPA ili iendane sambamba na malengo ya utekelezaji wa uchumi wa bluu.

7. Katika kuimarisha utendaji wa wafanyakazi, Programu imewapatia wafanyakazi 36 mafunzo ya muda mfupi kwa pamoja (group training) na 11 wamepatiwa mafunzo ya mmoja mmoja. Pia, kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imefanya utafiti wa Mwenendo wa Mitaji Binafsi (PCF) kwa mzunguko wa 13 ambao hivi sasa upo katika hatua ya kuandaa ripoti. Vile vile, imeanzisha Mfumo wa Kieletroniki "E-Office System" wa kupokea na kujibu barua pamoja na nyaraka nyengine za ki-ofisi kwa haraka.

8. Imefanikiwa kutangaza Visiwa Kumi (10) kwa ajili ya uwekezaji na tayari wameshajitokeza wawekezaji kwa visiwa hivyo. Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 261.5 ambazo ni mtaji wa makisio unaotarajiwa kuwekezwa katika visiwa hivyo. Aidha, Serikali imeanza mchakato wa

kutangaza visiwa vyengine 10 kwa Uwekezaji ambapo visiwa 6 tayari wameshatokeza wawekezaji na matarajio ni kukusanya malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 5.8.

9. Imekamilisha utaratibu wa kuanzisha Ofisi ya Benki ya Watu Wa Zanzibar (PBZ) kwa lengo la kurahisisha huduma za kibenki kwa uwekezaji, hatua ambayo imeimarisha zaidi ile dhana ya Kituo Kimoja cha Utoaji wa Huduma za Uwekekzaji. Pia, katika kuhakikisha huduma bora za uwekezaji ndani ya maeneo huru zinapatikana, inaendelea na kazi ya kujenga miundombinu mbali mbali na kuendelea na kazi ya kuanza kujenga ukuta katika maeneo huru ya Viwanda, Amaani.

**51. Mheshimiwa Spika;** Program kwa mwaka wa fedha 2022/23, imepanga kuimarisha sekta ya uwekezaji kwa kutanua fursa za uwekezaji kwenye visiwa; kuimarisha upatikanaji wa ardhi ya akiba; kuimarisha utoaji wa huduma kupitia kituo cha 'One Stop Center"; kuimarisha maeneo huru ya Uwekezaji na kutangaza fursa za uwekezaji ndani na nje ya nchi.

**52. Mheshimiwa Spika**; Ili Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naiomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Bilioni Kumi na Saba,

Milioni Mia Nane Thamanini na Sita na Laki Nane (Tshs.17,886,800,000) kwa ajili ya ruzuku ya mshahara na kazi za maendeleo.

**53. Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu **(PA0801)** ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Bilioni Nane, Milioni Mia Sita Hamsini na Tano, Laki Nne Kumi na Saba na Arubaini na Moja (Tshs.8,655,417,041); Hadi tarehe 31 Machi, 2022, Programu iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Sabini na Nane, Laki Nane Ishirini Elfu, Mia Sita Arobaini (Tshs.1,378,820,640) ambayo ni sawa na asilimia 16 ya makadirio.

## 5.2 PROGRAMU KUU PA0802: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI KATIKA UCHUMI NA UWEKEZAJI.

### 5.2.1 Programu ndogo SA080201: Utawala na Uendeshaji.

**54. Mheshimiwa Spika**; Programu Ndogo ya (SA080201) ya Utawala na Uendeshaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Uendeshaji na Utumishi za na Kukuza uwezo wa Afisi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa

mwaka wa fedha 2021/2022, Program imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Imesimamia kufanya malipo ya Safari za ndani kumi na mbili (12) za viongozi na Watendaji wa Afisi kwenda Pemba, Dar es salaam na Dodoma, imefanya matengenezo na imelipia bima gari Katibu Mkuu na kusimamia ununuzi wa mafuta kwa ajili ya ufuatiliaji wa kazi mbali mbali. Pia, Programu inaendelea kugharamia malipo ya Umeme, gharama za Ulinzi na kugharamia washiriki wa Maonyesho ya Sherehe za Mapinduzi.

2. Imesimamia ununuzi wa vifaa vya kuandikia, samani za Afisi na vitendea kazi kwa lengo la kumarisha utendaji kazi. Vile vile, imelipia mashine ya alama ya vidole kwa ajili ya mahudhurio ya Wafanyakazi na imefanya ukarabati wa ukumbi wa mkutano pamoja na Afisi nyengine kwa kuwekea samani na vitendea kazi vipya.

3. Imefanya malipo ya posho na ada ya mafunzo ya muda mfupi kwa wahasibu wawili (2) yaliyofanyika Morogoro na wafanyakazi wanne (4) wameshiriki mafunzo ya huduma kwa Wateja yaliofanyika Unguja. Pia, imefanya manunuzi ya vitendea kazi kwa Walinzi, Sare kwa Madereva wa Afisi na matengenezo ya Mfumo wa umeme na maji.

**55. Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Program ya Utawala na Uendeshaji itaendelea kusimamia Maslahi ya Wafanyakazi kama vile malipo ya mishahara, posho la likizo, malipo ya saa za ziada, malipo ya ubani kwa wafiwa pamoja na kuandaa na kufatilia malipo ya viinua mgongo kwa Wastaafu wetu; itaendelea kutoa mafunzo ya ndani, zoezi la Upimaji Utendaji kazi kwa Wafanyakazi kwa kila mwaka, kuimarisha mazingira ya Afisi nje na ndani; itaandaa Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimali watu.

**56. Mheshimiwa Spika,** ili program ndogo ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naiomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya Shillingi Millioni Mia Saba Ishirini na Tatu, Laki Tatu Arubaini na Nane Elfu (Tshs.723,348,000) kwa kazi za kawaida na mishahara.

### 5.2.2 Programu Ndogo SA080202: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi

**Lengo Kuu:** Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Sera, Mipango, Programu na Tafiti za Wizara zinazohusiana na Uchumi na Uwekezaji.

**57. Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ndogo ya (SA080202) ya

Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Afisi imeweza kutekeleza shughuli zifuatazo:-

1. Inaendelea na hatua ya uandaaji wa Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar ambapo rasimu ya muongozo huo tayari imeshapitiwa na Wadau mbali mbali wa taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali na kutoa maoni yao ya kuboresha Muongozo huo. Maoni hayo yamewasilishwa kwa Mtaalamu Muelekezi ili aweze kuyazingatia katika rasimu hiyo na kuikamilisha kwa kuanza kufanyiwa kazi.

2. Imeanza mchakato wa kuifanyia mapitio Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005 ambapo ipo katika hatua ya kumtafuta Mtaalamu Elekezi atakayeiandaa Sera Mpya ya Uwekezaji itakayokwenda sambamba na Sera za Nchi za Kiuchumi, kuimarisha uwekezaji nchini na mabadiliko yaliyopo Zanzibar na ulimwenguni kwa ujumla.

3. Imefanya ziara ya Kikazi Dodoma kushiriki Mkutano wa kujadili Mpango Kazi wa Mashirikiano baina ya Tanzania na Serikali ya Uingereza ambapo zimekubaliana kuimarisha mazingira ya Biashara na Uwekezaji kupitia Mpango wa Serikali kwa Serikali maarufu G2G. Serikali imeitaka Serikali ya Uingereza kuimarisha mashirikiano katika Maeneo ya Kodi, Sera na Sheria pamoja na maeneo ya Uwekezaji.

4. Katika kukamilisha utekelezaji wa Mpango huo Afisi imefanya vikao na taasisi mbali mbali ikiwemo ZRB, TRA, ZNBC, Fedha na Mwanasheria Mkuu kuangalia ni maeneo gani Zanzibar inaweza kunufaika na mashirikiano hayo. Zanzibar imeweka msisitizo kwenye kujengewa uwezo katika kukusanya na kuchambua kodi kielektroniki, Mafunzo ya Wanasheria juu ya kusuluhisha migogoro ya wawekezaji, kuimarisha One Stop Center ya ZIPA na kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Uwekezaji pamoja na kuzifanyia kazi changamoto za kisera na kisheria zinazokwamisha biashara na uwekezaji nchini. Afisi inatarajia kufanya kikao na Ubalozi wa Uingereza Aprili 2022 kukubaliana juu ya maeneo hayo.

5. Imefanya ziara ya kukusanya Taarifa za Miradi mbalimbali inayosimamiwa na PPP na ZIPA kwa lengo la kuangalia aina ya miradi inayoweza kuingia katika miradi ya PPP ili kuweza kuandaa Andiko la Mradi (Concept note) na kuweza kutafuta Wawekezaji Binafsi kushirikiana na Serikali katika kutekeleza Miradi hiyo ya Maendeleo. Pia, kuangalia maeneo ya uwekezaji. Katika ziara hiyo Taasisi na Maeneo mbali mbali ya Uwekezaji yalitembelewa ikiwemo Kamisheni ya Utalii na Mambo ya Kale Wilaya ya Kusini Pemba; Kamisheni ya Utalii na Mambo ya Kale – Development of the House of Persians-Ras Mkumbuu Ndagon Wilaya ya Kusini; Kamisheni ya Utalii na Mambo ya Kale – Development of Mkamandume – Pujini Kusini;

Maeneo mengine ni Fundu Lagoon Wambaa Wilaya ya Kusini; Kamisheni ya Utalii na Mambo ya Kale: Development of the Ruins of the Ancient Town Ole Mandani Wilaya ya Kaskazini; Chamanangwe Industrial Park Wilaya ya Kaskazini; Baraza la Mji Wete Development of Children Recreation Facilities: Kinyasini Wilaya ya Kaskazini; Rubber Plantation: Finya Wilaya ya Kaskazini na Micheweni Free Economic Zone – Block B Wilaya ya Kaskazini

Changamoto kubwa iliyojitokeza ni kwamba Maeneo mengi ya Kihistoria kwa Upande wa Pemba hayana Hati Miliki (Tittle deed) za maeneo na kupelekea baadhi ya maeneo hayo kuwa na Mgongano na mzozo na jamii inayoyazunguka. Pia, baadhi ya maeneo ya kihistoria kukosekana kwa picha halisi za maeneo ya kihistoria na miundo mbinu kama barabara inahitaji kuboreshwa. Miradi mingi ni mizuri na yenye kutekelezeka kwa mashirikiano ya pamoja baina ya PPP na Serikali na kupelekea kuweza kuingiza Pato la Taifa kwa ujumla.

6. Imeratibu utayarishaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji ikiwemo, ripoti ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 - 2025 na ripoti maalum zilizohitajika kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2021 zinazohusiana na uchumi na uwekezaji ambazo huwekwa pamoja na kupelekekwa sehemu husika.

7. Imelipia gharama za safari za ndani ya nchi (Pemba na Tanzania Bara) kwa wafanyakazi ili kushiriki katika vikao na shughuli mbali mbali za Afisi zinazohusiana na Uchumi na Uwekezaji. Pia, imefanya ziara na Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi kukagua miradi ya Uwekezaji Kisiwani Pemba na Unguja. Miongoni mwa changamoto iliyobainika ni kukosekana kwa miundombinu ya barabara katika Hoteli ya Kitalii ya Fundu Lagoon Pemba inayopelekea usumbufu mkubwa kwa wageni hadi kubidi kutumia njia ya bahari kufika hotelini hapo na uharibifu wa mazingira katika eneo la Uwekezaji Fumba.

8. Imeandaa taarifa za utekelezaji kama vile Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, taarifa za Bajeti na taarifa za utekelezaji wa shughuli za Afisi.

**58. Mheshimiwa Spika**; Program kwa mwaka wa fedha 2022/23, imepanga kuendelea na mapitio ya Sera ya Uwekezaji, Kuchapisha nakala za Sera ya PPP na Uwekezaji; Kufanya tafiti za Afisi kwa mujibu wa Agenda za Utafiti; Kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi ya Afisi; Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi; Kuimarisha Mfumo wa TEHAMA na upatikanaji wa habari na taarifa za Afisi; Kuimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

59. **Mheshimiwa Spika**; Ili Programu Ndogo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Tafiti za Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23, naiomba Baraza lako kuidhinisha jumla Shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Tatu, Laki Moja Hamsini na Nne (Tzs.313,154,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

### 5.2.3 Programu Ndogo SA080203: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba.

60. **Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya (SA080203) ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa upande wa fungu A08 Programu hii haijaingiziwa Bajeti. Hivyo haijatekeleza kitu kwa upande wa Pemba.

61. **Mheshimiwa Spika**; Program kwa mwaka wa fedha 2022/23, inaendelea na kusimamia maslahi ya wafanyakazi, utoaji wa mafunzo,elimu kwa jamii, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa sera na sheria ya ZIPA na PPP, kuandaa taarifa za utekelezaji na kufanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini za Afisi pamoja na kuripoti utekelezaji wake.

62. **Mheshimiwa Spika**; Ili program ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/23 naliomba Baraza lako kuidhinisha Shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Tatu, Laki Moja Hamsini na Nne (Tshs.313,154,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

63. **Mheshimiwa Spika;** Programu Kuu **(PA0802)** ya Uendeshaji na Utumishi wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ilikadiriwa matumizi ya Shilingi Milioni Mia Nne na Saba, Laki Tatu Arubaini na Tano Elfu (Tshs.407,345,000); Hadi tarehe 31 Machi, 2022, Programu iliidhinishiwa matumizi ya Shilingi Mia Mbili Sabini na Nne Elfu (Tshs.274,000,000) ambayo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio.

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI) NA FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

### *6.1 FUNGU A07 KAZI NA UWEZESHAJI*

64. **Mheshimiwa Spika,** Ili Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) iweze kutekeleza Programu zake

kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naiomba Baraza lako iidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Thalathini na Nne, Milioni Mia Nane Sabini, Laki Moja Ishirini Elfu (Tshs.34,870,120,000). Kati ya hizo Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tatu Tisini na Nane, Laki Nane Thamanini Elfu (Tshs.2,398,880,000) ni Mishahara; Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Moja Thalathini na Nane, Laki Mbili Arubaini Elfu (Tshs.3,138,240,000) ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Thalathini na Tatu (Tshs.1,733,000,000) kwa ajili ya ruzuku na Shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Sita (Tshs.27,600,000,000) kwa ajili ya matumizi ya miradi ya Maendeleo.

**65.** **Mheshimiwa Spika;** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ni kama ufuatao:- Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Ishirini na Tisa (Tshs.1,529,000,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote; Shilingi Bilioni Ishirini na Tisa, Milioni Mia Tatu Sabini na Saba, Laki Mbili na Elfu Saba (Tshs.29,377,207,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tisa Sitini na Tatu, Laki Tisa na Kumi na Tatu Elfu (Tshs.3,963,913,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji (**Kiambatanisho nambari 4(a) kinahusika)**.

**66. Mheshimiwa Spika,** Pia, Afisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) inatarajiwa kukusanya mapato ya Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Moja (Tshs.2,100,000,000) kutokana na Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi (**Kiambatanisho nambari 4(b) kinahusika)**.

### *6.2 FUNGU A08 UCHUMI NA UWEKEZAJI*

**67. Mheshimiwa Spika,** Ili Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naiomba Baraza lako iidhinishe jumla ya Shilingi Bilioni Kumi na Tisa, Milioni Mia Saba Kumi na Nne, Laki Nane Arobaini Elfu (Tshs.19,714,840,000). Kati ya hizo Shilingi Milioni Mia Mbili Sitini na Mbili, Laki Mbili Sabini Elfu (Tshs.262,270,000) ni Mishahara; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Tano, Laki Saba Sabini Elfu (Tshs.1,565,770,000) ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za Kawaida; Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Saba Thamanini na Sita na Laki Nane (Tshs.2,786,800,000) ni kwa ajili ya Ruzuku na Shilingi Bilioni Kumi na Tano na Milioni Mia Moja (Tshs.15,100,000,000) kwa ajili ya matumizi ya miradi ya Maendeleo.

68. **Mheshimiwa Spika;** Mgawanyo wa fedha hizo kwa Programu za Fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ni kama ufuatao:- Shilingi Bilioni Kumi na Nane, Milioni Mia Tatu Sitini na Tano, Laki Moja Thamanini na Nne Elfu (Tshs.18,365,184,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu Arubaini na Tisa, Laki Sita Hamsini na Sita Elfu (Tshs.1,349,656,000) zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji (**Kiambatanisho nambari 5 kinahusika)**.

## 7.0 HITIMISHO

69. **Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Watendaji mbali mbali ikiwemo taasisi za Serikali, taasisi za kiraia na Washirika wa Maendeleo. Miongoni mwa Washirika wa Maendeleo tunaofanya kazi nao ni pamoja na ILO, MIVARF, UNDP, COSTECH, Milele Foundation, FAO, Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia, Afisi inafanya kazi na Taasisi za Kiraia na inazishukuru Taasisi zote inazoshirikiana nazo. Vile vile, tunazishukuru taasisi zote za kifedha,

ikiwemo Benki ya PBZ na CRDB kwa mashirikiano yao mazuri na Afisi yetu.

70. **Mheshimiwa Spika;** Napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari vinavyoshirikiana nasi katika kuelimisha jamii juu ya shughuli tunazozifanya. Vyombo vya habari vimechangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Afisi yetu kujulikana na jamii. Sitaweza kuvitaja kimoja kimoja lakini navishukuru vyote kwa ujumla. Aidha, Napenda kuwashukuru wote wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu kwa njia moja au nyengine; nawaomba waendelee kuwa nasi katika kufanikisha malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. Vile vile, nawashukuru kwa dhati Wawekezaji wote waliowekeza na wale wote waliooneshа nia ya kuja kuwekeza nchini. Tunawakaribisha sana.

71. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwashukuru Watendaji wote wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuanzia Makatibu Wakuu wa Uchumi na Uwekezaji Ndugu Habiba Hassan Omar; Katibu Mkuu Kazi na Uwezeshaji Ndugu Khadija Khamis Rajab; Ofisa Mdhamini Pemba; Kamishna wa Kazi; Wakurugenzi na Watendaji wote kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawaomba waboreshe umoja na mshikamano tulionao katika kuwahudumia wananchi wetu na wawekezaji nchini.

72. **Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe na Wajumbe wote wa Kamati kwa Miongozo, hekima, busara na maoni mnayotupatia katika kuimarisha utendaji wa shughuli zetu za kila siku. Nakuomba wewe na Wajumbe wako kuwa Mabalozi wazuri kwa Wananchi kuwashajiisha na kuhakikisha wananufaika na Mkopo wa fedha za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zilizoaininshwa na Mheshimiwa Rais ili waweze kuimarisha shughuli zao za kujipatia kipato na kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi.

73. **Mheshimiwa Spika**; Naomba kutoa hoja.

..................................................

**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA**
**(MBM)**
**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**
**ZANZIBAR.**

# 8.0 VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho Nambari 1

### FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

### MUHTASARI WA MAPATO YALIYOKUSANYWA KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI 2022

| Kasma | Vyanzo vya Mapato | Bajeti ya Mwaka | Makadirio ya Miezi Tisa Julai 2021 hadi Machi 2022 | Makusanyo halisi ya Miezi Tisa Julai 2021 hadi Machi 2022 | Asilimia ya Makadirio ya Miezi Tisa | Asilimia ya Makadirio ya Mwaka 2021/2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | (%) | (%) |
| 1422036 | Ada ya Usajili wa Vyama vya Ushirika | 30,000,000 | 23,500,000 | 70,799,000 | **301** | **236** |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika | 30,000,000 | 24,000,000 | 26,699,750 | **111** | **89** |
| 1422071 | Ukaguzi wa Usalama na Afya maeneo ya Kazi | 630,000,000 | 472,700,000 | 100,135,000 | **21** | **16** |
| 1422075 | Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi | 290,000,000 | 218,500,000 | 23,450,000 | **11** | **8** |
| 1422011 | Ada ya Vibali vya Kazi kwa Wataalam wa Kigeni | 1,005,626,000 | 762,126,000 | 774,695,338 | **102** | **77** |
| 1422012 | Ada ya Uhakiki wa Mikataba | 850,000,000 | 654,300,000 | 58,528,881 | **9** | **7** |
| | **JUMLA** | **2,835,626,000** | **2,155,126,000** | **1,054,307,969** | **49** | **37** |

**Kiambatanisho Nambari 2(a)**

## FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2022

| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO YA MIEZI TISA (JULAI -MACHI) 2021/2022 | MATUMIZI MENGINEYO (OC) " A" | MATUMIZI YA MISHAHARA "B" | MATUMIZI YA MAENDELEO "C" | JUMLA YA FEDHA ZILIZOINGIZWA JULAI - MACHI 2021/2022 "A+B+C" | ASILIMIA YA FEDHA JULAI - MACHI. 2021/2022 (%) | ASILIMIA YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022 (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI** | **2,236,900,000** | **1,402,393,070** | **179,493,500** | **526,606,630** | **-** | **706,100,130** | **50** | **32** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja | 1,496,900,000 | 1,226,083,070 | 82,060,600 | 526,606,630 | - | 608,667,230 | 50 | 41 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | 120,000,000 | 96,310,000 | 59,192,700 | - | - | 59,192,700 | 61 | 49 |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha | 620,000,000 | 80,000,000 | 38,240,200 | - | - | 38,240,200 | 48 | 6 |
| **PROGRAMU KUU YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | **6,584,676,000** | **1,729,845,977** | **234,587,450** | **524,895,486** | **-** | **759,482,936** | **44** | **12** |
| Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 318,207,000 | 292,062,727 | 31,306,500 | 90,817,185 | - | 122,123,685 | 42 | 38 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika | 666,750,000 | 547,407,500 | 63,358,950 | 271,174,380 | - | 334,533,330 | 61 | 50 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 5,599,719,000 | 890,375,750 | 139,922,000 | 162,903,921 | - | 302,825,921 | 34 | 5 |
| **PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI** | **6,691,916,640** | **4,167,227,978** | **632,019,050** | **1,531,871,850** | **947,520,000** | **3,111,410,900** | **75** | **46** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti | 3,276,705,640 | 1,576,917,500 | 62,513,650 | 125,664,145 | 947,520,000 | 1,135,697,795 | 72 | 35 |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 2,142,686,000 | 1,562,931,230 | 371,805,400 | 686,059,135 | - | 1,057,864,535 | 68 | 49 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba | 1,272,525,000 | 1,027,379,248 | 197,700,000 | 720,148,570 | - | 917,848,570 | 89 | 72 |
| **JUMLA KUU** | **15,513,492,640** | **7,299,467,025** | **1,046,100,000** | **2,583,373,966** | **947,520,000** | **4,576,993,966** | **63** | **30** |

**Kiambatanisho 2(b)**

## FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2022

| PROGRAMU | BAJETI YA MWAKA | MAKADIRIO JULAI HADI MARCH 2022 | MATUMIZI MENGINEYO OC | MATUMIZI YA MISHAHARA | MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO | JUMLA OC NA MISHAHARA NA FEDHA ZA MAEDELEO | ASILIMIA JULAI HADI MARCH |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi** | **9,707,312,180** | **8,656,417,041** | **95,000,000** | **1,283,820,640** | **0** | **1,378,820,640** | **16** |
| Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi | 1,407,203,485 | 1,087,585,520 | 95,000,000 | 104,734,510 | 0 | 199,734,510 | **18** |
| Programu Ndogo ya Kushajiisha Uwekezaji wa ndani na nje ya nchi | 8,300,108,695 | 7,568,831,521.00 | | 1,179,086,130 | 0 | 1,179,086,130 | **16** |
| **Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji** | **587,150,000** | **407,345,000** | **274,000,000** | **0** | **0** | **274,000,000** | **67** |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa rasilimali na huduma za utawala | 449,545,000 | 302,950,000 | 227,630,000 | 0 | 0 | 227,630,000 | **75** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti | 137,605,000 | 104,395,000 | 46,370,000 | 0 | | 46,370,000 | **44** |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli Pemba | 0 | | 0 | | | 0 | **0** |
| **JUMLA KUU** | **10,294,462,180** | **9,063,762,041** | **369,000,000** | **1,283,820,640** | **0** | **1,652,820,640** | **18** |

**Kiambatanisho Nambari 3(a) na 3(b)**

## UTOAJI WA MIKOPO KWA MWAKA WA 2021/22 MFUKO WA UWEZESHAJI

| Na. | Wilaya | Idadi ya mikopo | Ya wanawake | Ya wanaume | Fedha zilizotoka | Ajira za kudumu/moja kwa moja | Ajira za Muda | **Ajira zote** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkoani | 40 | 23 | 17 | 29,000,000 | 40 | 104 | 144 |
| 2 | Chake Chake | 49 | 29 | 20 | 44,500,000 | 49 | 122 | 171 |
| 3 | Micheweni | 35 | 21 | 14 | 26,000,000 | 35 | 97 | 132 |
| 4 | Wete | 38 | 23 | 15 | 34,000,000 | 38 | 95 | 133 |
| | **Jumla Pemba** | **162** | **96** | **66** | **133,500,000** | **162** | **418** | **580** |
| 5 | Magharibi A | 20 | 11 | 9 | 20,100,000 | 20 | 51 | 71 |
| 6 | Magharibi B | 25 | 15 | 10 | 24,650,000 | 25 | 63 | 88 |
| 7 | Kati | 14 | 8 | 6 | 16,000,000 | 14 | 36 | 50 |
| 8 | Kusini | 14 | 6 | 8 | 13,700,000 | 14 | 33 | 47 |
| 9 | Kaskazini A | 13 | 7 | 6 | 9,800,000 | 13 | 31 | 44 |
| 10 | Kaskazini B | 18 | 10 | 8 | 14,700,000 | 18 | 49 | 67 |
| 11 | Mjini | 20 | 12 | 8 | 20,700,000 | 20 | 48 | 68 |
| | **Jumla Unguja** | **124** | **69** | **55** | **119,650,000** | **124** | **311** | **435** |
| | **Jumla Kuu** | **286** | **165** | **121** | **253,150,000** | **286** | **729** | **1,015** |

# Kiambatanisho Nambari 3(b)

## MAREJESHO YA MIKOPO KWA KIPINDI CHA JULAI 2021 HADI MACHI, 2022

| Wilaya | Julai 2021 | Agosti 2021 | Septemba 2021 | Oktoba 2021 | Novemba 2021 | Disemba 2021 | Januari,2022 | Februari, 2022 | Machi, 2022 | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Chake Chake** | 4,109,000 | 4,410,000 | 7,398,000 | 4,020,500 | 4,398,000 | 4,042,000 | 4,773,000 | 2,568,000 | 2,478,000 | **38,196,500** |
| **Mkoani** | 4,046,000 | 5,014,000 | 5,019,000 | 3,427,000 | 3,382,000 | 4,314,000 | 2,826,000 | 2,566,000 | 2,798,000 | **33,392,000** |
| **Wete** | 2,993,000 | 7,030,000 | 5,274,000 | 2,922,000 | 3,293,000 | 4,104,000 | 3,522,600 | 2,220,000 | 2,800,000 | **34,158,600** |
| **Micheweni** | 3,293,500 | 4,130,500 | 2,896,000 | 3,321,500 | 4,019,500 | 3,751,000 | 4,498,000 | 2,130,000 | 4,289,000 | **32,329,000** |
| **JUMLA NDOGO** | **14,441,500** | **20,584,500** | **20,587,000** | **13,691,000** | **15,092,500** | **16,211,000** | **15,619,600** | **9,484,000** | **12,365,000** | **138,076,100** |
| **Mjini** | 2,864,000 | 3,692,000 | 3,404,000 | 2,615,000 | 2,071,000 | 2,360,000 | 2,845,000 | 3,383,000 | 3,287,000 | **26,521,000** |
| **Magharibi "A"** | 2,020,000 | 4,315,000 | 1,385,000 | 2,400,000 | 2,445,000 | 2,680,000 | 3,355,000 | 4,395,000 | 3,765,000 | **26,760,000** |
| **Magharibi "B"** | 4,185,000 | 6,294,000 | 3,578,000 | 2,630,000 | 2,800,000 | 3,390,000 | 2,850,000 | 4,840,000 | 3,765,000 | **34,332,000** |
| **Kaskazini "A"** | 1,890,000 | 2,665,000 | 2,180,000 | 2,987,000 | 2,100,000 | 3,625,000 | 2,675,000 | 3,390,000 | 2,980,000 | **24,492,000** |
| **Kaskazini "B"** | 1,710,000 | 2,015,000 | 1,010,000 | 3,110,700 | 3,105,000 | 1,920,000 | 3,285,000 | 3,360,000 | 3,608,000 | **23,123,700** |
| **Kati** | 2,860,000 | 3,335,000 | 3,059,000 | 3,050,000 | 3,390,000 | 2,795,000 | 3,260,000 | 3,945,000 | 3,500,000 | **29,194,000** |
| **Kusini** | 3,875,000 | 1,815,000 | 1,455,000 | 2,657,600 | 2,510,000 | 2,895,000 | 2,375,000 | 4,470,000 | 3,298,000 | **25,350,600** |
| **JUMLA NDOGO** | **19,404,000** | **24,131,000** | **16,071,000** | **19,450,300** | **18,421,000** | **19,665,000** | **20,645,000** | **27,783,000** | **24,203,000** | **189,773,300** |
| **JUMLA KUU** | **33,845,500** | **44,715,500** | **36,658,000** | **33,141,300** | **33,513,500** | **35,876,000** | **36,264,600** | **37,267,000** | **36,568,000** | **327,849,400** |

**Kiambatanisho Nambari 4**

## KAMPUNI 11 ZA FEED THE FUTURE ZILIZOSAJILIWA

| NA. | JINA LA KAMPUNI | ME | KE | JUMLA | NAMBA YA USAJILI | NAMBA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | AL- JAMIL PARTNERSHIP | 1 | 2 | 3 | Z 0000136435 | 0629-775441 |
| 2. | HIMAA ENTREPRISES | 3 | - | 3 | Z 0000137851 | 0774-054713 |
| 3. | JASNAF ENTREPRISES | - | 3 | 3 | Z 0000136578 | 0773-033716 |
| 4. | MAMBO SIRI | - | 3 | 3 | Z 0000136523 | 0778-596549 |
| 5. | MVIVU HAVUNI | - | 4 | 4 | Z 0000136446 | 0772-646771 |
| 6. | WAPENDANAO ENTREPRISES | - | 2 | 2 | Z 0000136204 | 0718-764053 |
| 7. | PIONER ENTREPRISES | - | 3 | 3 | Z 0000136347 | 0772-859636 |
| 8. | PROSPECT FOR YOUTH | - | 3 | 3 | Z 0000136215 | 0779-233540 |
| 9. | SHIMMER GROUP | - | 2 | 2 | Z 0000136897 | 0773-871660 |
| 10. | VUNILLA GROWING | 2 | 3 | 5 | Z 0000136875 | 0778-288982 |
| 11. | TRUEST ENTREPRISES | 1 | 3 | 4 | Z 0000136480 | 0622-825816 |

**Kiambatanisho Nambari 5(a)**

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA FUNGU LA A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)**

| Programu | MATUMIZI YA KAWAIDA (OC) | MISHAHARA | RUZUKU | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| **Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote** | | | **1,529,000,000** | | **1,529,000,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha | | | 150,000,000 | | 150,000,000 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini | | | 150,000,000 | | 150,000,000 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja | | | 1,229,000,000 | | 1,229,000,000 |
| **Programu Kuu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **896,000,000** | **677,207,000** | **204,000,000** | **27,600,000,000** | **29,377,207,000** |
| Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | | 116,605,000 | 204,000,000 | | 320,605,000 |
| Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika | 336,000,000 | 351,277,000 | | | 687,277,000 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 560,000,000 | 209,325,000 | | 27,600,000,000 | 28,369,325,000 |
| **Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **2,242,240,000** | **1,721,673,000** | | | **3,963,913,000** |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti | 490,000,000 | 168,403,000 | | | 658,403,000 |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 1,120,000,000 | 653,313,000 | | | 1,773,313,000 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 632,240,000 | 899,957,000 | | | 1,532,197,000 |
| **JUMLA KUU** | **3,138,240,000** | **2,398,880,000** | **1,733,000,000** | **27,600,000,000** | **34,870,120,000** |

**Kiambatanisho Nambari 5 (b)**

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

| **PEMBA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KASMA** | **MAELEZO** | **MAKADIRIO 2022-2023** | **MAKISIO 2023-2024** | **MAKISIO 2024-2025** |
| 1422012 | Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi | 25,000,000 | 40,000,000 | 80,000,000 |
| 1422036 | Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika | 20,000,000 | 25,000,000 | 40,000,000 |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma | 20,000,000 | 25,000,000 | 40,000,000 |
| 1422071 | Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi | 25,000,000 | 40,000,000 | 75,000,000 |
| | **JUMLA PEMBA** | **90,000,000** | **130,000,000** | **235,000,000** |

| **UNGUJA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KASMA** | **MAELEZO** | **MAKADIRIO 2022-2023** | **MAKISIO 2023-2024** | **MAKISIO 2024-2025** |
| 1422036 | Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika | 50,000,000 | 60,000,000 | 65,000,000 |
| 1422037 | Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma | 30,000,000 | 45,000,000 | 50,000,000 |
| 1422075 | Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira za Nje | 36,800,000 | 50,000,000 | 70,000,000 |
| 1422011 | Vibali vya Kazi kwa Wataalamu wa Kigeni | 1,243,200,000 | 1,138,267,116 | 1,258,815,414 |
| 1422012 | Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi | 200,000,000 | 550,012,452 | 774,997,038 |
| 1422071 | Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi | 450,000,000 | 595,000,000 | 700,000,000 |
| | **JUMLA UNGUJA** | **2,010,000,000** | **2,438,279,568** | **2,918,812,452** |
| | **JUMLA KUU** | **2,100,000,000** | **2,568,279,568** | **3,153,812,452** |

**Kiambatanisho Nambari 6**

## MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWA FUNGU LA A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

| Programu | MATUMIZI YA KAWAIDA (OC) | MISHAHARA | RUZUKU | MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| **Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma** | **313,154,000** | **165,230,000** | **2,786,800,000** | **15,100,000,000** | **18,365,184,000** |
| Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma | 313,154,000 | 165,230,000 | | | 478,384,000 |
| Programu Ndogo ya Kushajiisha Uwekezaji wa ndani na nje ya nchi | | | 2,786,800,000 | 15,100,000,000 | 17,886,800,000 |
| **Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** | **1,252,616,000** | **97,040,000** | | | **1,349,656,000** |
| Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji | 626,308,000 | 97,040,000 | | | 723,348,000 |
| Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti | 313,154,000 | | | | 313,154,000 |
| Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | 313,154,000 | | | | 313,154,000 |
| **JUMLA KUU** | **1,565,770,000** | **262,270,000** | **2,786,800,000** | **15,100,000,000** | **19,714,840,000** |